SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**'House Boy'** mwenye tuhuma za kumuua bosi aitwa kutubu

UKURASA 2



**Huyu ndiye mtaalamu Yogo mwenye mikono ya dhahabu**

UKURASA 20

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Januari 2, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580813
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Askofu awa mkali mapenzi jinsia moja

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**TFS YATAKA BEI YA GESI IPUNGUZWE**
WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umezishauri mamlaka zinazohusika na masuala ya nishati...

UKURASA WA 17
**ASKOFU TUTU AFANYIWA MAZISHI YA KITAIFA**
MAZISHI ya kitaifa ya mwanaharakati aliyepinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, Askofu Mkuu Desmond Tutu...

## Kiongozi dini atoa angalizo vita vya corona Mwaka Mpya

UKURASA 2



Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, akibariki waumini wa kanisa hilo, wakati akiingia kanisani kuendesha misa ya kuupokea Mwaka Mpya wa 2022 juzi, katika Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma, Ngokolo mjini Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**



## Rekodi mpya yawekwa katika makusanyo TRA

UKURASA 3

**MICHEZO** **NABI ATARAJIA MAKUBWA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Askofu atoa angalizo Corona Mwaka Mpya

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, Mhashamu Lazarus Msimbe, amewataka Watanzania kuendelea kuliombea taifa kwa Mungu dhidi ya UVIKO-19 na kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kukabiliana na mapambano ya ugonjwa huo.

Kiongozi huyo alitoa wito huo katika mahubiri yake kwa waumini wa kanisa hilo wakati wa ibada ya kuukaribisha Mwaka Mpya 2022 iliyofanyika kwenye Kanisa Kuu la Mtakatifu Patrice mjini Morogoro usiku wa kuamkia jana.

Wakati wa ibada hiyo tahadhari zote za kujikinga na maambuziki ya ugonjwa huo zilizingatiwa kwa waumini, ikiwamo kukaa kwa kupeana nafasi.

Askofu Msimbe alisema ni wajibu kwa Watanzania kuendelea kuliombea taifa kwa Mungu dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 na kuunga mkono juhudi zote zinazochukuliwa na serikali dhidi ya ugonjwa huo.

Askofu Msimbe pia aliwataka waumini wa kanisa hilo hususani wa Jimbo la Morogoro na Watanzania wote kuendelea kudumisha amani iliyopo na upendo ili kuboresha ustawi wa jamii.

Aliwataka waamini kuwapokea jirani zao bila masharti yoyote kwa kuwa Mungu anaonyesha nia yake ya kumfariji kila mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano wake.

Kutokana na dosari za vitendo hivyo vinavyodhalilisha utu na heshima ya binadamu, alisema kanisa linaamini linaweza kuchangia kwa namna mbalimbali katika kuifanya familia ya binadamu kuwa na utu zaidi kupitia watu binafsi au jumuiya.

**HOFU YA UVIKO-19**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Jacob Paulo Ole Mameo, kwenye mahubiri yake kwa waumini wa kanisa hilo alisisitiza Watanzania kutokuogopa uwapo wa ugonjwa wa UVIKO-19 na badala yake waungane na serikali katika kukabiliana nao.

Pia alisisitiza umuhimu kwa wananchi kujenga upendo miongoni mwao na kudumisha amani iliyopo ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Baadhi ya waumini kutoka makanisa hayo, kwa nyakati tofauti walitoa wito kwa jamii kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Waumini hayo pia walimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua mbalimbali alizochukua za kupambana na ugonjwa huo.

# Askofu ayakemea mapenzi jinsia moja

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, amekemea mapenzi na ndoa za jinsia moja, akionya kuwa vitendo hivyo ni laana mbele za Mungu.

Alibainisha hayo juzi kwenye misa ya mkesha wa kuuaga mwaka 2021 na kuupokea mwaka mpya 2022 kwenye Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma lililoko Ngokolo mjini Shinyanga.

Alisema watu wanaoendekeza mapenzi na ndoa za jinsia moja wanamkashifu Mungu na wanajipatia laana, akiwataka watubu dhambi zao na kuacha vitendo hivyo mara moja.

"Chimbuko la mafanikio katika maisha ya binadamu ni kumtanguliza Mungu kwa kila jambo na kuacha dhambi ikiwamo ya mapenzi na ndoa za jinsia moja.

"Na ndiyo maana Hayati Rais John Magufuli alikuwa akitukumbusha kila mara tumtangulize Mungu kwa kila kitu, ili tupate baraka,"alisema Askofu Sangu.

Kiongozi huyo wa kiroho pia alikemea uharibifu wa mazingira, akionya kuwa vitendo hivyo navyo ni dhambi na vimekuwa vikisababisha mabadiliko ya tabianchi na hata kusababisha mvua kutonyesha. Aliwataka wanadamu kumruhusu Roho Mtakatifu atawale maisha yao kwa kuwa ndiye chimbuko la amani, furaha na upendo.

Askofu Sangu pia aliwataka waumini wajenge tabia ya kusaidia wahitaji na kuacha kuwanyanyapaa watu wenye virusi vya Ukimwi na wanaougua maradhi ya ukoma.

Pia aliwasisitiza wanadamu wawe na tabia ya kushukuru kwa kila jambo, hata kwa mambo ambayo hawapendezwi nayo na siyo kulaumu kwa kuwa kila kinachofanyika duniani kimepangwa na Mungu, hivyo wanapaswa kujifunza kuombana msamaha wanapokoseana.

Baadhi ya waumini waliokuwa kwenye mkesha huo, kwa nyakati tofauti walisema wanamshukuru Mungu kwa kuwavusha salama mwaka uliopita huku wakiahidi kutenda mema zaidi mwaka huu na kujitahidi kutimiza malengo yao ambayo wamejiwekea.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na waumini mara baada ya kumalizika kwa Misa Takatifu ya sherehe za Bikira Maria mama wa Mungu pamoja na kumshukuru Mungu kwa mwaka mpya 2022 katika kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Paulo wa Msalaba Jimbo Kuu la Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# 'House Boy' anayetuhumiwa kumuua bosi wake aitwa kutubu

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

PADRI Patrick Mahanda wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu John, amemtaka mfanyakazi wa kazi za ndani 'House Boy', aliyetajwa kwa jina moja la Boniface (18), anayedaiwa kumuua kwa kumpiga na jembe b sosi wake, Jane Dewasi, ajisalimishe na atubu kwa kuwa damu yake itamlilia.

Kiongozi huyo wa kiroho alitoa rai hiyo juzi alipohubiri wakati wa ibada ya mazishi ya Jane, aliyedaiwa kuuawa na mfanyakazi wake huyo anayedaiwa kutoroka baada ya kufanya mauaji hayo.

Alisema kuwa vifo vipo vinavyotokana na ajali, kuugua au hata kufia usingizini lakini kifo cha Jane (68) ni cha kulazimisha, hivyo damu yake inamlilia aliyeimwaga bila hatia.

"Ajisalimishe na atubu apate msamaha, sisi tumeshamsamehe kulingana na matakwa ya maandiko. Mama Jane ni mcha Mungu, ni mpole hata ukimpiga kofi harudishi, inauma sana. Ninaomba na wanafamilia tutoe msamaha kwa muuaji na maisha yaendelee," alisema Padri Mahanda.

Alisema kuwa Jane ameondoka kwa maumivu makali na damu yake inalia kwa kuwa haijamwagika yenyewe bali imemwagwa na mwanadamu.

"Kijana huyo awe Dar au Singida, lakini damu ya mama huyu inamlilia kwa kumfuata huko," Padri Mahanda alisema.

Aliongeza kuwa binadamu wamekuwa tishio kwa wenzao badala ya kuwa msaada, akifafanua kuwa usalama umekuwa shakani kutokana na unyama uliokithiri miongoni mwa binadamu.

Katika ibada hiyo, kiongozi huyo wa kiroho pia aliwakumbusha madereva wa pikipiki, maarufu bodaboda, kuendesha vyombo vyao kwa kufuata alama za usalama barabarani kwa kuwa wanabeba roho za watu.

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo, alidai kuwa Jane alimchukua kijana Boniface kanisani wiki moja iliyopita baada ya kuona bango lake la kuomba msaada na kupewa kazi kutokana na maisha magumu yaliyokuwa yanamkabili.

"Mtoto huyo alifika kuomba apatiwe chakula na kazi, alikuwa amedhoofika kwa njaa na ndipo Jane akamchukua akafanye kazi kwa nia ya kumsadia," alisema muumini huyo aliyeomba hifadhi ya jina lake.

## HABARI KITAIFA

# Wafurahia mitandao ya kijamii kwa kuboresha biashara, kipato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Wajasiriamali na wafanyabiashara Zanzibar wamesema teknolojia ya mitandao ya kijamii imesaidia kukuza biashara zao na kupata kipato.

Waliyasema hayo jana wakati wakizungumza katika mkutano kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii uliofanyika kwa njia ya mtandao (zoom) ulioandaliwa na Jukwaa la Vijana Zanzibar kupitia ufadhili wa taasisi ya habari ya Internews.

Zuhra Ali, mmoja wa washiriki wa mkutano huo, alisema mitandao ya kijamii imerahisisha kufanya biashara hasa baada ya wimbi la Corona kuibuka na kuathiri shughuli mbalimbali ikiwamo mikusanyiko ya watu kibiashara na kijamii.

Alisema biashara mitandaoni imeshamiri baada ya kuibuka kwa wimbi la corona na kwamba kwa sasa mfumo wa biashara kupitia mitandao ya kijamii umezoeleka kwa jamii.

"Mitandao ya kijamii imeturahisishia sisi wajasiriamali kuuza bidhaa zetu kupitia mitandao hiyo ambayo imetujengea umaarufu," alisema.

Mjasiriamali huyo alizishauri kampuni za simu za mkononi kupunguza gharama za intaneti kwa kuwa bila njia hiyo ya mawasiliano hawawezi kuitumia mitandao ya kijamii.

Akiwasilisha mada kuhusu faida za mitandao ya kijamii katika mkutano huo, Khelef Nassor, alisema mitandao ya kijamii imetoa fursa za ajira kwa vijana.

Khelef alisema baadhi ya vijana wamejiajiri kupitia mitandao ya kijamii ikiwamo kurusha maudhui ya kihabari kupitia mitandao hiyo.

Aliwataka vijana kuitumia vizuri mitandao hiyo ili iwapatie faida lakini pia kuzingatia mila na desturi katika matumizi yake.

Naye Mkurugenzi wa Jukwaa la Vijana Zanzibar (ZYF) Maulid Suleiman, alisema taasisi hiyo itaendelea kutoa elimu kwa vijana kuhusu matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii ili kuleta maendeleo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimpongeza Rehema Hamisi ambaye amejifungua mtoto wa kike katika Kituo cha Afya cha Nandagala wilayani Ruangwa, mkoani Lindi katika wodi ya Mama na Mtoto kwenye kituo hicho, Desemba 31, 2021. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Rekodi mpya yawekwa katika makusanyo TRA

**Na Sanula Athanas**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imetangaza makusanyo yake kwa nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22, yaani kutoka Julai 2021 hadi Desemba 2021, mapato ya Desemba yakiweka rekodi mpya ya makusanyo ya mwezi tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo takriban miaka 27 iliyopita.

Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu TRA, katika taarifa yake kwa umma jana, alibainisha kuwa wamefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. trilioni 11.11 katika kipindi hicho cha miezi sita, ikiwa ni sawa na asilimia 98 ya lengo la makusanyo ya Sh. trilioni 11.302.

Alibainisha kuwa makusanyo hayo ni ongezeko la Sh. trilioni 1.87 kulinganishwa na kiwango cha makusanyo cha Sh. trilioni 9.24 kilichokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/21, akifafanua kuwa ni ongezeko la ukuaji wa makusanyo wa asilimia 20.2.

"TRA inapenda kuutaarifu umma kuwa katika kipindi cha mwezi Desemba 2021 imefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. trilioni 2.51 kati ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 2.29.

"Makusanyo haya ya mwezi Desemba 2021 yana ufanisi wa asilimia 109. Pamoja na makusanyo haya kuvuka lengo, ndicho kiwango cha juu kukusanywa kwa mwezi tangu kuanzishwa kwa mamlaka (mwaka 1995)," Kidata alibainisha.

Alisema kuwa katika kipindi cha nusu mwaka, mwenendo wa ulipaji kodi kwa hiari na uhusiano baina ya mamlaka na walipakodi umeimarika kwa kiwango cha kuridhisha.

Kamishna Mkuu huyo alisema TRA inatoa pongezi na shukurani kwa walipakodi wote na wadau mbalimbali kwa kujitoa kwa dhati katika kuwezesha kufikiwa kwa kiwango hicho cha makusanyo, hivyo kuiwezesha mamlaka kuweka rekodi mpya ya ukusanyaji mapato nchini tangu kuanzishwa kwake.

"Mioyo yenu ya kujitoa ni tunu kubwa kwa taifa na kielelezo cha uzalendo uliotukuka kwa nchi yetu, husussan ukizingatia kuwa kodi ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya serikali yanayotumika kuendesha shughuli za ulinzi, ujenzi wa miundombinu, utoaji huduma za afya, elimu, maji na huduma nyinginezo za jamii.

"Kwa namna ya pekee mamlaka inapenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa miongozo aliyoitoa kwa mamlaka kutoa huduma zinazozingatia uadilifu, weledi na uwajibikaji ili kukidhi matarajio ya walipakodi na wananchi kwa ujumla kwa kuwapatia walipa kodi mazingira mazuri ya kuzalisha mali na rahisi ya ulipaji kodi," alisema.

Muda mfupi baada ya kuapishwa kushika nafasi aliyonayo sasa, Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, alisisitiza kuwa moja ya mambo atakayomsaidia Rais Samia ni kuhakikisha makusanyo ya TRA yanakuwa ya wastani wa Sh. trilioni mbili kwa mwezi.

Kidata pia alibainisha kuwa pamoja na mafanikio waliyoyapata, bado iko haja ya kuongeza kiwango cha makusanyo kwa kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari kwa walipakodi.

Alisema mamlaka inawakumbusha walipakodi na wadau wasiozingatia sheria, kanuni na taratibu za ulipaji kodi, kubadilika ili kuwaepusha kulipa riba, adhabu, kesi na usumbufu wanaoweza kuupata.

Kamishna Mkuu huyo alisema kuwa wakati wakiuanza mwaka 2022, wanaomba wadau wote wazingatie wauzaji wote wa bidhaa na huduma mbalimbali wanatoa risiti sahihi za kielektroniki (EFD) katika kila mauzo wanayofanya.

Alisema jambo lingine la kuzingatiwa ni wanunuzi wote wadai risiti sahihi za kielektroniki katika kila ununuzi wa bidhaa au huduma wanayopatiwa, kwa kuwa kupitia kudai risiti sahihi ya bidhaa au huduma wanayopatiwa wanakuwa wametoa mchango mkubwa kwa taifa.

Kidata pia alikumbusha walipakodi kuwasilisha ritani sahihi na kulipa kodi stahiki kwa wakati, wazalishaji na waingizaji wa bidhaa nchini zinazotozwa ushuru wa bidhaa, kuzingatia matumizi sahihi ya stempu za ushuru wa bidhaa.

Pia walipakodi kulipa madeni yao ya kodi kwa wakati, walipakodi na wadau kuendelea kuhudhuria mafunzo mbalimbali yanayotolewa na TRA juu ya elimu ya kodi na matumizi ya mifumo ya usimamizi wa kodi ili kujijengea uwezo.

"Tunapenda kuwatakia walipakodi na Watanzania wote heri na fanaka tele katika mwaka mpya 2022.

Ni matumaini yetu kuwa mwenendo wa ulipaji kodi na uhusiano mzuri baina ya mamlaka na walipakodi utaendelea kuimarika na hivyo kupelekea kufikiwa kwa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambalo ni Sh. trilioni 22.733," alisema.

Kamishna Kidata alisema TRA inawahakikishia walipakodi wote na umma kwa ujumla kuwa imejizatiti katika kuboresha utoaji huduma, kuongeza elimu ya kodi, kurahisisha mifumo ya uwasilishaji ritani na ulipaji kodi, hatua zitakazochochea kuongeza uelewa na kurahisisha ulipaji kodi na hivyo kuongeza kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari.

## Serikali yajipanga kukabili majanga

**Na Lawrence Matongo,** DODOMA

SERIKALI imesema imedhamiria kuendelea kuchukua hatua stahiki dhidi ya majanga na maafa nchini kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa cha Kisasa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alibainisha hayo juzi alipotembelea na kukagua Kituo cha Oparesheni na Mawasiliano ya Dharura kilichoko katika ofisi hiyo jijini Dodoma kwa lengo la kupokea taarifa na hatua zinazochukuliwa katika kuboresha utendaji wa kituo hicho.

Alisema kuwa kati ya mambo mazuri yaliyofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Menejimenti ya Maafa katika mwaka 2021 ni ujenzi wa mradi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa cha Kisasa kinachojengwa eneo la Nzuguni 'B' jijini Dodoma.

"Ofisi ya Waziri Mkuu tunajivunia na kunashukuru serikali kwa kutupatia fedha za ujenzi wa mradi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa ambacho kitasaidia kuimarisha uwezo wa usimamizi wa maafa katika sekta zote nchini kwa ajili ya maendeleo endelevu," alisema.

Waziri Mhagama aliongeza: "Ujenzi wa kituo hicho ni dhamira ya serikali katika kuhakikisha inazingatia namna njema ya hatua za kuchukua tahadhari dhidi ya majanga na maafa yanapojitokeza."

Alisema kuwa katika kutekeleza mpango huo, serikali imeendelea na azma ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa nchini kwa kuingiza tena mpango wa ujenzi wa kituo hicho katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020 hadi 2025 katika Ibara ya 107 kipengele (h) ikiwa na lengo la kuhakikisha vyombo vinavyoshughulika na maafa vinakuwa na mpango wa utayari wa kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea.

Alisema kituo hicho pia kitasaidia kuimarisha mfumo wa usimamizi wa maafa na kuwezesha uwapo wa vifaa na zana za kisasa katika utoaji wa huduma za usimamizi wa maafa nchini, kuwa na mfumo wa kisayansi wa kufuatilia mwenendo wa majanga na kutoa maelekezo ya hatua za kuchukua kwa wakati kwa ajili ya tahadhari za awali, kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kuzuia na kupunguza madhara ya majanga pamoja na kujiandaa, kukabili na kurejesha hali baada ya maafa.

Baada ya ziara hiyo ya kukagua kituo hicho, Waziri Mhagama aliwataka wadau kutoka katika sekta mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya majanga na maafa kuwa na mfumo wa kanzidata ili kujua namna walivyorejesha hali katika maeneo yaliyokumbwa na majanga na maafa.

# Mwambe aonya siasa chafu Masasi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MBUNGE wa Masasi mkoani Mtwara, Geoffrey Mwambe, amesema iwapo siasa za makundi zinazoendelea wilayani hapa hazitadhibitiwa, zitarudisha nyuma jitihada za maendeleo zinazofanywa na wadau mbalimbali.

Mwambe ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), alisema hayo jana katika kikao cha wadau wa maendeleo wilayani Masasi kilichofanyika kwa ajili ya uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji maendeleo. Kikao hicho kilifanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi.

Alisema ni jambo la aibu kuona bado wako baadhi ya watu wanaojiita wanasiasa wanaacha kuunganisha nguvu ili kuleta maendeleo na kutumia muda mwingi kuendekeza siasa makundi.

"Uchaguzi mkuu umekwisha lakini bado wako baadhi ya watu wanaendelea na uchaguzi tena wanakaa na kuwachafua viongozi ambao wako madarakani kwa lengo la kutaka kurudisha nyuma jitihada za maendeleo," alisema.

Mwambe alisema iwapo siasa za makundi zitaendelea kushika kasi ndani ya wilaya ya Masasi katika majimbo yote ya Masasi, Lulindi na Ndanda, nguvu zote zinazotumika za kimaendeleo zitakuwa bure.

"Siasa za uchaguzi Masasi bado hazijakwisha licha ya uchaguzi wa mwaka 2020 kupita. Wapo baadhi ya watu wanatumia nguvu kubwa kutaka kutukwamisha, hawa tusiwape nafasi," alisema Mwambe.

Alisema ziko jitihada kubwa na mipango mizuri ya maendeleo inayowekwa na kutekelezwa kwa ajili ya Masasi lakini huenda malengo yasifikiwe kwa sababu ya hali ya kisasa iliyoko Masasi.

Mwambe alisema wana Masasi ni lazima wakae na kutafakari kwa kina na kutowaunga mkono watu wachache ambao wana dhamira mbaya ya kutaka kuirudisha nyuma Masasi kimaendeleo.

Alisema serikali itaendelea kuwahudumia wananchi wa Masasi kwa kuwapatia huduma za msingi ili waendelee kufurahia matunda ya serikali yao.

Mkuu wa wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema mpango wa maendeleo uliozinduliwa jana, utasaidia kuleta maendeleo wilayani hapa kwa kasi kubwa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Jenista Mhagama (kushoto) akiangalia taarifa na hatua zinazochukuliwa katika kuboresha utendaji wa kituo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TFS yataka bei ya gesi ipunguzwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umezishauri mamlaka zinazohusika na masuala ya nishati ya gesi, kuangalia namna ya kuuza nishati hiyo kwa bei nafuu ili wananchi wengi waitumie na kuachana na matumizi ya mkaa unaosababisha uharibifu wa mazingira.

Akizungumza na wenyeviti wa vijiji mara baada ya kumalizika kwa ziara ya kutembelea Hifadhi ya Msitu wa Chenene Magharibi, Mhifadhi wa Misitu wilayani Chamwino, Byela Kahangwa, alisema juzi kuwa kutokana na matumizi ya mkaa, wananchi wamekuwa wakiharibu mazingira ili kupata nishati ya mkaa kwa ajili ya kupikia.

Alisema ukuaji wa Mji wa Dodoma umefanya mahitaji ya nishati ya mkaa kuongezeka na hivyo kusababisha uharibifu wa msitu huo.

Mhifadhi huyo alisema uharibifu huo umeisukuma TFS kuzitaka mamlaka zinazohusika na biashara ya gesi, kuhakikisha bei ya nishati hiyo inakuwa chini ili jamii iweze kutumia kama mbadala wa matumizi ya kuni.

Alisema kuwapo kwa nishati mbadala inayopatikana kwa bei nafuu kutaiua biashara ya mkaa, hivyo kuhifadhi mazingira.

"Hii inaweza kutekelezeka kwa kukaribisha wawekezaji mbalimbali katika Mji wa Dodoma na kwenye vijiji vinavyozunguka msitu ili watu wageukie fursa nyingine tofauti na ilivyo sasa, fursa pekee ni ukataji miti kwa ajili ya utengenezaji wa mkaa," alisema Kahangwa.

Alizitaja kero zinazokwaza uhifadhi wa msitu huo ni pamoja na utegemezi mkubwa wa msitu kama chanzo cha nishati ya mkaa, wafugaji kuwa sehemu ya uvamizi wa msitu na kushauri mageti ya vijijini ya ukaguzi wa mazao ya misitu yabadilishe mrengo wa kukusanya maduhuli.

"Kutoza Sh. 2,000 kwa gunia la mkaa au kipande cha mbao hakutoshi, taratibu za uvunaji wa mazao ya misitu zifuatwe kikamilifu na ambaye hajafuata utaratibu achukuliwe hatua za uharibifu wa mazingira," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda na uongozi wa serikali ya vijiji waliazimia kuwa hadi Machi mwaka huu kuwe kumeundwa Kikosi Maalumu kwa ajili ya kudhibiti uharibifu unaondelea katika hifadhi hiyo.

Waliwataka wenyeviti wa vijiji kuendelea kuelimisha wananchi wasikate mkaa eneo la hifadhi kwa kuwa msitu huo ni 'ubavu' wa Jiji la Dodoma kwa kuwa upo karibu na chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya jiji hilo.

"'Hali ni mbaya kwa kweli, wimbi kubwa la watu wanakuja kutafuta maeneo ya kulima katika vijiji hivi kwa kuwa kuna mvua ya kutosha," alisema Mkuu wa Wilaya hiyo.

Wenyeviti wa Vijiji akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Babayu, Eliya Ndagala, amekiri kuwapo kwa uharibifu katika hifadhi hiyo na kudai kuwa wageni ndio wanaochangia kwa kiasi kibwa uharibifu huo.

Msitu wa Hifadhi Chenene Magharabi umehifadhiwa kisheria kwa Gazeti la Serikali Na. 382 la Mei 12, 1989, ukiwa na mipaka yenye urefu wa kilometa 84.

# Jafo ataka miti Mji wa Serikali

**Mji wa Serikali**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ametoa wiki tatu kwa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuanza upandaji wa miti kando ya barabara zilizoko Mji wa Serikali eneo la Mtumba jijini Dodoma.

Dk. Jafo alitoa maelekezo hayo juzi alipozuru kikazi katika eneo hilo kwa ajili ya kukagua hali ya mazingira na kuipongeza TARURA kwa hatua iliyofikia katika ujenzi wa barabara hizo.

"Hapa serikali imewekeza takriban Sh. bilioni 89 kwa ajili ya kujenga miundombinu hii muhimu ya barabara. Sasa jukumu langu ni kuhakikisha eneo hili linakidhi matakwa ya kimazingira ikiwamo upandaji wa miti. Maelekezo yangu nataka mtumie mvua hii inayoanza kunyesha kupanda miti," aliagiza.

Waziri Jafo alisema barabara hizo zimejengwa kwa kiwango kinachotakiwa kwa kuwa na mifereji ambayo inasaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo unaoweza kutokea pindi mvua inaponyesha.

Alishauri ipandwe miti ya matunda ili kuweka mandhari nzuri ya Mji wa Serikali na kuwa haoni sababu ya kuchelewa kuanza kwa zoezi hilo.

Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na Jamii wa TARURA, Dk. Veronica Mirambo, alisema upo mpango wa upandaji miti katika barabara zote zilizojengwa katika eneo hilo.

Alisema kuwa shughuli iliyobaki ni kufukia ardhi iliyochimbwa wakati wa ujenzi pamoja na upandaji wa miti na majani ili kurejesha hali ya mazingira katika hali yake.

Ofisa Mazingira wa Jiji la Dodoma, Alo Mfinanga, alisema Idara ya Mazingira kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kati inaendelea na kampeni ya 'kuikijanisha' Dodoma.

Aliongeza kuwa miongoni mwa maeneo inayoyafanyia kazi ni barabara kadhaa na kuwa wanawashirikisha wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za fedha kushiriki katika upandaji miti.



Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Herihuruma Mabelia (kushoto), akiwaongoza baadhi ya wananchi waliojitokeza katika mkesha wa Mwaka Mpya uliofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana kushoto kwake ni Askofu wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches, Dk. Godfrey Emmanuel. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwarobaini uhaba wa maji shuleni wanaswa

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

WANAFUNZI wa shule za msingi wilayani Babati mkoani Manyara wataanza kunufaika na ujenzi wa madarasa sambamba na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua iliyojengwa na wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na serikali ili kukabiliana na uhaba wa maji pamoja na magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza juzi mjini Babati wakati akikabidhi madarasa hayo yaliyojengwa na wadau wa maendeleo, Mkurugenzi wa Shirika la Maisha Capacity Development Opportunity (MCDO), Jasson Kahembe, alisema wamejenga jumla ya madarasa tisa katika Shule ya Msingi Sawe wilayani Babati.

Alisema lengo la ujenzi huo uliojumuisha miundombinu ya kuvuna maji ya mvua, ni kupunguza uhaba wa maji na mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu na UVIKO -19.

"Ninafahamu wanafunzi wanakuwa wengi kwa sababu watu wanahamia kwa wingi eneo hili na sisi tumejenga ili tuwe na mikondo miwili awamu ya kwanza kupunguza msongamano darasani na huku tukitimiza moja ya masharti ya kujikinga na UVIKO-19," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kabla ya kujenga madarasa hayo, walifanya uchunguzi kwenye shule nyingi na kubaini uhaba wa maji walionao ambao hawapaswi kuwa nao kwa sababu wana madarasa yaliyoezekwa kwa bati na yanafaa kutumika kuvuna maji ya mvua.

Alisema kuwa baada ya kubaini hilo, waliamua kujenga madarasa mapya na kuweka miundombinu ya kuvuna maji ili waondokane na uhaba huo na kuwapunguzia gharama za kununua maji.

Diwani wa Maisaka, Abdulrahaman Kololi, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Babati na Mbunge wa Babati, Paulina Gekul, walilipongeza shirika hilo kusaidia jamii inayowazunguka.

Wadau wa elimu, Sixbert Joseph na Yoha Jastin, walisema wameweka pia matanki ya kuhifadhi maji ili kuhakikisha msimu wa masika na kiangazi shule zinakuwa na akiba ya maji.

Alisema MCDO wanashirikiana na serikali, halmashauri na wananchi wanaotoa michango ya mawe na matofali kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa na haikwami.

000000

# Mkuu wa Mkoa atoa wiki mbili za uondoshaji taka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha John Mongela ametoa wiki mbili kwa maofisa mazingira wa mkoa huo kuhakikisha wanaondoa takataka zinazozagaa kando ya barabara kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (KIA) kwenda Arusha na Babati hadi Makuyuni.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Arusha alipopokea madarasa 105, viti na meza 5,250, mradi uliotekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo wa mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Alisema Mkoa wa Arusha lazima uwe mfano wa usafi wa mazingira kutokana na kupokea asilimia 85 ya watalii wanaofika nchini kuangalia vivutio vilivyopo.

"Sasa unakuta kando ya barabara hizi hasa KIA kuja Arusha zimezagaa chupa, foili za vyakula na mifuko, hali ambayo haileti taswira nzuri kwa wageni wetu. Lazima tuanze mwaka mpya kwa kubadilika kwenye kudumisha usafi wa mazingira," aliagiza.

Mongela aliagiza kukamatwa wanaotupa taka hizo hasa wenye mabasi ambao kwa kiasi kikubwa huchangia uchafuzi huo kupitia abiria wao. Aliagiza kila Jumamosi ya mwanzo wa mwezi kila mtu kusafisha eneo lake la makazi na biashara ili kila mahali pawe safi.

Kiongozi huyo alisema sambamba na hilo, pia atawafuatilia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoani Arusha kuhakikisha wanaboresha barabara za mkoa huo ili ziendane na hadhi ya kitalii.

"TARURA na TANROADS wanachangia uchafuzi wa mazingira kwa sababu wanaacha barabara zetu hasa mitaani hazifai, hili nitakufa nalo na kesho (jana) mtu asifungue biashara yake bila kuanza kufanya usafi kwanza. Nataka mwaka mpya tuanze na usafi wa mazingira," alisema.

Mongela aliitaka Halmashauri ya Jiji hilo kuhakikisha inaweka vizimba vya kutupa taka na kusimamia vyema wanaochukua taka hizo kwenda kuzitupa dampo ili wananchi wasikusanye taka wakakosa pa kuzipeleka.

Kwa mujibu wa Mongela, Jiji la Arusha lazima pia lipande miti na kutengeneza barabara nzuri za kupanda Mlima Suye ili uwe chanzo cha mapato kwa wanaopanda kufanya mazoezi.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda, alisema madarasa mapya 105 yaliyojengwa, yatawezesha wanafunzi 11,427 kuingia kidato cha kwanza mwaka huu na kufanya jumla ya madarasa 764 ya sekondari na msingi.

"Hivyo, madarasa haya ni ukombozi mkubwa kwa watoto wetu maana hata wanafunzi wa darasa la kwanza 16,440 nao wataingia darasani," alisema.

Alisema madarasa hayo yataleta uwiano wa watoto 50 kukaa darasani, badala ya 80 walivyokuwa wakikaaa awali kabla ya madarasa hayo, hali itakayoweka salama katika nyakati za maambukizi ya UVIKO -19.

Mkurugenzi wa Halmshauri ya Jiji la Arusha, Dk. John Pima, aliishukuru serikali kuwapatia Sh. bilioni 2.1 zilizowawezesha kukamilisha kwa wakati madarasa mapya 105, viti na meza kwa ajili ya wanafunzi 50 kwa kila darasa.

Hata hivyo, uwiano unaotakiwa kisera ni wanafunzi 45 kwa kila chumba cha darasa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tubadilike kifikra, tufanye kazi kwa bidiii Mwaka Mpya

**WATANZANIA** juzi usiku waliungana na mataifa mengine duniani kuupokea Mwaka Mpya wa 2022 kwa namna tofauti baadhi wakiwa kwenye nyumba za ibada kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwavusha salama kutoka mwaka uliopita.

Pia katika ibada hizo, walimwomba Mungu awape baraka na kuwafanikisha katika mambo mbalimbali pamoja na kuwaepusha dhidi ya majanga kama vile maradhi ikiwamo ugonjwa wa corona ambao umeendelea kushika kasi katika mataifa mbalimbali.

Wakati ibada za kuuaga na kuukaribisha Mwaka Mpya zikifanyika, wako wengine waliokuwa wakisherehekea wakiwa nyumbani, kazini na kwenye kumbi za starehe wakijipongeza kwa kuvuka salama.

Kama ilivyo ada kwa baadhi ya watu, wako waliokaa, kutafakari na kufanya tathmini juu ya mambo waliyokuwa wamepanga kuyafanya katika mwaka uliopita kwa kuangalia walivyotekeleza mipango yao, changamoto walizokutana nazo na kushindwa kufikia malengo hatimaye kujipanga zaidi ili kufanikisha mambo yao kwa mwaka ulioanza.

Ni dhahiri kwamba katika mwaka uliopita, kulikuwa na matatizo au vikwazo mbalimbali ambavyo viliathiri familia, jamii na taifa kwa ujumla kiuchumi na kijamii ikiwamo baadhi ya mambo kutokufanyika kama ilivyopangwa.

Jambo kubwa la kukumbukwa zaidi ni watu wengi kupoteza maisha kwa sababu mbalimbali kama vile maradhi ikiwamo corona na ajali za barabarani. Kwa ujumla yako mengi ambayo yaliitikisa nchi na dunia hususani mtikisiko wa kiuchumi uliosababishwa na janga la corona.

Pamoja na hayo yote, jambo la muhimu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuvusha salama kuufikia mwaka 2022. Kama wahenga wasemavyo yaliyopita si ndwele tugange yajayo, vivyo hivyo tufunge ukurasa wa 2021 na kuutazama kwa namna chanya ukurasa mpya wa 2022.

Haina maana kwamba tusahau yote yaliyofanyika mwaka uliopita bali tuelekeze nguvu na mawazo yetu zaidi kwa mwaka mpya katika kufanya ubunifu juu ya mambo ya maendeleo huku mwaka uliopita ukiwa marejeo na tathmini ya kuelekea katika ustawi wa familia, jamii na taifa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Watanzania tunapaswa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kila mtu katika sehemu na nafasi yake ili kujiletea maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Kuanzia ngazi ya familia, taasisi na serikali, inatakiwa kuandaliwa mipango madhubuti ambayo itawawezesha watu kuitekeleza na hatimaye kujipatia maendeleo.

Kwa mantiki hiyo, tabia ya kufanya mambo kwa mazoea inapaswa kuachwa na kila mtu kuwa mbunifu na kutumia juhudi na maarifa katika kufanya kazi ili kupata mafanikio katika kila jambo linalofanyika kwa njia halali. Pia kila mtu anapaswa kutumia muda alionao kwa kufanya kazi badala ya kufanya mambo yasiyo na tija.

Tunasema hivyo kwa sababu baadhi ya watu waliofanikiwa kimaisha duniani, siri kubwa ni matumizi sahihi ya muda, fursa zinazowazunguka, kupanga mipango yao na kuitekeleza pamoja na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Siri nyingine iliyosababisha wakafikia mafanikio ni kuwa na nidhamu na kila kitu wanachokifanya ikiwamo matumizi ya rasilimali.

Ni wazi kwamba kama kila mtu atafanya kazi kwa kujituma, kuheshimu muda, kuwa na nidhamu na kuacha kufanya mambo kwa mazoea, Watanzania tutapiga hatua kimaendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kasi ya kupata chanjo corona iongezeke 2022

**SAFARI** yenye milima na mabonde ya mwaka 2021 hatimaye imemalizika huku ikiwa imeacha mengi yakiwamo ya kufurahisha na mengine ya kuhuzunisha. Hatimaye sasa umeanza mwaka mpya wa 2022.

Miongoni mwa matukio makubwa ya kuhuzunisha yaliyotokea mwaka 2021, ni kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, lakini pia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa wa corona.

Kifo cha Rais Magufuli kimeshazungumzwa na kujadiliwa kwa mapana na marefu kutokana na uzito wake, lakini pia kuna suala la corona ambalo kwa mara ya kwanza mwaka 2021 Tanzania iliagiza chanjo ya ugonjwa huo.

Baada ya chanjo kuletwa nchini, Rais Samia Suluhu Hassan aliizindua Julai, mwaka huo, kwa kuchanjwa kisha ikasambazwa mikoa yote ili Watanzania wachanjwe kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo.

Hadi Desemba 18, mwaka jana, ni watu zaidi ya milioni 1.2 nchini ambao walikuwa tayari wameshapata chanjo kamili ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Mikoa inayoongoza kwa kufanya vizuri katika utoaji chanjo ya ugonjwa huo ni Ruvuma, Mwanza, Dodoma, Kagera na Mara, huku mikoa ya Manyara, Njombe, Singida, Iringa na Songwe ikitajwa kufanya vibaya kwa kujikongoja.

Kwa idadi hiyo ya watu waliochanjwa, ni wazi kwamba mwaka 2022 kuna haja ya kuongezeka kwa kasi ya chanjo kutokana na ukweli kwamba bado Tanzania inanyemelewa na ugonjwa huo.

Kwa mfano, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema idadi nyingi ya sampuli zinazopokewa katika Maabara Kuu ya Taifa, zinaonyesha kuongezeka kwa ugonjwa huo nchini. Anasema hadi sasa idadi ya sampuli zinazopokewa katika Maabara Kuu ya Taifa, zimeongezeka kutoka 14 kwa siku hadi kufikia 47, hali ikiashiria kuwa ni ongezeko la maambukizi.

Kuhusu hali ya wagonjwa wa corona, anasema, katika kila idadi ya watu 10, saba ni wale ambao hawajachanjwa, na wengine ni wale wanaozidiwa na magonjwa mengine kama shinikizo la damu, kisukari na uzee.

Pamoja na hayo, Dk. Gwajima anafafanua kuwa kasi ya kujikinga na maambukizi bado ni ndogo, licha ya kuwa wananchi wanaendelea kuchanja, na kwamba bado wanahitaji msukumo.

Serikali pia ilishatoa mwongozo wa kudhibiti ugonjwa huo kupitia misongamano katika jamii, bila kuathiri shughuli za kiuchumi, toleo la kwanza linaweka wazi jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mwongozo huo unaelekeza kila mtu kuvaa barakoa katika vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, huku vyombo vya ulinzi na usalama vikitakiwa kusimamia utekelezaji mwongozo huo.

Hata hivyo, kwa mwaka uliopita, kumekuwapo na uzembe wa kutozingatia mwongozo huo, kufuatia kutokuwa na mwitikio wa uzingatiaji vigezo vya tahadhari, ikiwamo katika uvaaji barakoa kwenye baadhi ya maeneo.

Kwenye baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam, bado watu wanaendelea kukusanyika kama kawaida bila ya hatua sahihi za tahadhari na pia kwenye vyombo vya usafiri kama daladala na kuna wakati wanajazana kupita kiasi, huku hata katika safari ndefu nako kukishuhudiwa hatua sahihi za udhibiti kutozingatiwa.

Hali hiyo pia ipo kwenye masoko, stendi za daladala na za mabasi yaendayo safari ndefu, bado kumeshuhudiwa msongamano mkubwa wa watu pasipo kuchukuliwa tahadhari sahihi dhidi ya ugonjwa huo.

Mwaka 2022 ungefaa kuwa wa mabadiliko, kwa kila mmoja kuchukua hatua sahihi za kuhakikisha anakuwa salama dhidi ya corona ikiwamo kuzingatia mwongozo, lakini pia kupata chanjo.

Vilevile uwe ni mwaka wa watu kuachana na elimu au taarifa potofu ambazo huwa zinatolewa na makundi mbalimbali ya kijamii kuhusu chanjo na kusababisha baadhi ya watu kutochanja ama kutozingatia mwongozo.

Jambo lingine la kuzingatia, ni maelekezo yanayotolewa na huku ikikumbushwa kuwa suala la chanjo lipo nchini kwa zaidi ya miaka 100 sasa, hivyo ni muhimu kuepuka watu wanaopotosha kuhusu chanjo.

## SAFU/MAKALA

### KWA MASLAHI YA TAIFA



Na Pascal Mayalla

**Kwa vile kuzaliwa, uhai na kifo ni vitu vilivyoko kwenye mamlaka ya juu kuliko uwezo wetu, hatuwezi kuuliza sababu, bali tunaweza kujadili yatokanayo. Hivyo kifo cha JPM ni moja ya majanga makubwa yaliyolikumba taifa letu mwaka 2021 kuhalalisha kuuita mwaka 2021 ulikuwa wa majanga kwa Tanzania.**

# Mwaka Mpya 2022 Watanzania tubadilike

JANA tuliuanza Mwaka Mpya wa 2022, hivyo nianze kwa kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya wasomaji wangu na Watanzania wenzangu, kama wazungu wasemavyo "Happy New Year'.

Wakati tukitakiana heri ya Mwaka Mpya, si vibaya tukiutafakari kidogo mwaka uliopita kwa Tanzania tumepitia wapi, tumekumbana na nini, tumejifunza nini, hivyo mwaka huu wa 2022 tunatakiwa kufanya nini.

Kwa kuanzia, mwaka 2021 ulikuwa wa majanga. Tuliuanza mwaka huku tukikabiliwa na janga la corona, ambalo sio tu tumewapoteza wapendwa wetu bali pia tuliwapoteza viongozi wetu. Si tu kupoteza nguvu kazi ya taifa, bali liliathiri shughuli mbalimbali za maendeleo na zinazotupatia kipato, utalii ikiwa moja ya sekta zilizoathirika kwa kiasi kikubwa.

Machi 17, 2021 tulimpoteza kiongozi wetu mkuu wa taifa, Rais John Pombe Magufuli. Ukiondoa msiba wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, msiba wa JPM ndio mkubwa wa kwanza kwa taifa kwa mkuu wa nchi kufariki dunia akiwa madarakani.

Kama ilivyo kila lenye mwanzo pia lina mwisho, vivyo hivyo kwa binadamu yeyote tangu ile siku anazaliwa, inajulikana wazi, kuna siku itafika na atakufa. Kila mtu atakufa, siku yake ikifika imefika. Hata mimi nitakufa, wewe utakufa na sote tutakufa, hivyo kifo kipo, tatizo ni mshtuko si kwa nini fulani amekufa.

Kwa vile kuzaliwa, uhai na kifo ni vitu vilivyoko kwenye mamlaka ya juu kuliko uwezo wetu, hatuwezi kuuliza sababu, bali tunaweza kujadili yatokanayo. Hivyo kifo cha JPM ni moja ya majanga makubwa yaliyolikumba taifa letu mwaka 2021 kuhalalisha kuuita mwaka 2021 ulikuwa wa majanga kwa Tanzania.

Kwenye hili janga la corona, hakuna familia ambayo haikuguswa. Hata mimi mwenyewe, wimbi la kwanza lilinitandika, dada yangu wa kuzaliwa Paula ikamchukua!. Wimbi la pili, ikanitandika tena, kaka yangu Peter, ikamchukua. Mimi nikachanja, wimbi la tatu limenipitia, kaka yangu aliyenitangulia Paul ikamchukua! Mimi naamini ni chanjo tuu ndiyo imesaidia, hivyo kuna wengi wametwaliwa wakiwamo baadhi ya viongozi wetu.

Kwa vile mpangaji ni Mungu, ndiye aliyetuletea JPM na kumfanya kuwa Rais wetu na ni Mungu aliyemchukua JPM na sasa Rais wetu ni Mama Samia, hivyo hayo ni mabadiliko yaliyofanywa na Mungu mwenyewe kwa Tanzania. Maana yake ni kwamba aliyeamua kufanya mabadiliko ya uongozi Tanzania ni Mungu. Hii ina maana Mama Samia, sasa ndiye mpango wa Mungu kwa Tanzania ya sasa.

Japo kifo cha JPM ni majanga pia kimeleta mabadiliko ya kumwingiza Samia, si kila majanga ni majanga. Majanga mengine yanatokea ili jamii ijifunze jambo fulani na kuchukua hatua kwa mabadiliko. Sote tunafahamu baadhi ya misimamo ya Rais Hayati Magufuli kuhusiana na baadhi ya mambo ikiwamo corona.

Lakini Samia amekuja na kubadili msimamo kuhusu corona kuwa ipo na tukachanje ili kujilinda. Sasa ni jukumu letu Watanzania katika umoja wetu, kwenda na mabadiliko chanya yoyote, hivyo mwaka huu wa 2022, uwe wa mabadiliko, Watanzania tubadilike.

Enzi za JPM, Tanzania tuligomea corona kutokana na msimamo wa kiongozi wetu mkuu na kweli tukaamini kwamba haipo. Lakini kiukweli corona imekula vichwa! Tena naamini, kuna baadhi ya vifo vilitokana na corona.

Sasa Samia kaingia, Tanzania tumeikubali corona ipo na tumekubali chanjo ambayo ni hiari, nashauri kwa mwaka huu wa 2022, chanjo ya corona iwe ni hiari ya lazima kwa baadhi ya kada wakiwamo wasafiri.

Enzi za JPM, alianzisha miradi mingi ya kimkakati na kutangaza kuwa tunaijenga kwa fedha za ndani huku tukikopa kwa siri, bila kusema tumekopa wapi na tunafanyia nini. Enzi hizo watu wote walinyamaza, leo kaingia Mama Samia kawa muwazi. Akikopa anasema tumekopa. Anataja kiasi kilichokopwa, anataja mkopo huo tunaufanyia nini.

Badala ya Mama Samia kupongezwa kwa kuwa muwazi, ndiyo kwanza baadhi ya watu wanapiga mayowe, deni la taifa kufika Sh. trilioni 70 na kusema mwisho nchi itauzwa! Wakati hizo Sh. trilioni 70 zikikopwa na awamu ya JPM walinyamaza, leo Mama amekuwa muwazi wanapiga kelele!. Mwaka 2022 tubadilike tuwe wawazi zaidi.

Kuna watu wanatoka makabila ya mfumo dume, hivyo kuongozwa na mwanamke kwao kunawapa shida, hivyo sasa kazi yao ni kila siku kutafuta makosa na kukosoa. Hata kwenye uumbaji, japo Mungu alimuumba mwanamume Adamu na kumfanya ndiye mtawala wa dunia, kiukweli Eva au Hawa ndiye alimtawala Adam.

Watanzania tubadilike, tukubali mwanamke ndiye anayetawala nyumba na dunia! Tubadilike tumpe Samia ushirikiano unaohitajika kuliletea maendeleo taifa letu. 2022 ni mwaka wa mabadiliko, Watanzania tubadilike.

**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

**Tunayaona yakijitokeza, mfano mzuri ni wa hivi karibuni, kumhusu 'Mwanaharakati Huru', ndugu yangu Cyprian Musiba, ambaye yamemkuta mahakamani kutokana na kauli zake alizopata kutoa siku za nyuma.**

# Vijana wa kitanzania kuna leo na kesho

USEMI maarufu wa hujafa hujaumbika, una maana kubwa sana kwamba umuhimu wa mtu hujibainisha, pale anapokuwa ameaga dunia. Hapo ndipo utasikia sifa kedekede, alikuwa hivi alikuwa vile.

Kabla hujafa huwezi kusikia sifa hizo, ingawa zingine huwa hasi na zingine chanya lakini ukiwa hai watakaa nazo kimya wakisubiri siku yako ya kufarakana na dunia yako na kwenda kuanza maisha mapya ahera.

Binadamu duniani tumegawanyika katika makundi mawili, yenye hisia na misimamo tofauti kuhusu maisha na kuhusu watu waishio duniani. Ndiyo sababu wewe ukimpenda fulani huyu atamchukia.

Mmoja anaweza kushangaa kwa nini huyu anampenda yule, halikadhalika huyu naye atamshanga kwa nini yule anampenda huyu, hii ni mitazamo na imani walizo nazo binadamu kuhusu mambo, vitu na watu.

Lakini tunajifunza hapa hapa kambi hizo mbili na hakuna anayeweza kumshurutisha huyu kuamini au kupenda lile. Ni matakwa binafsi yatokanayo na faragha ya kila mtu na kadri aaminivyo.

Tunayaona yakijitokeza, mfano mzuri ni wa hivi karibuni, kumhusu 'Mwanaharakati Huru', ndugu yangu Cyprian Musiba, ambaye yamemkuta mahakamani kutokana na kauli zake alizopata kutoa siku za nyuma.

Wako watu walizipenda na kuzishabikia bila kujali athari hasi zilizokuwa zikiwapata aliowashambulia. Lakini wako waliokuwa wakizifuriha na kuzishangilia na kuziona ndizo zenyewe hasa. Wakiziona chanya.

Alionekana katika tasnia ya habari kama shujaa kwa waliokuwa wanamkubali na kauli zake, akitamba kumtetea Rais John Magufuli na kujiapiza kuwa tayari kufa. Ikawa kama tamthiliya maarufu za Ertugrul na Sultani ambako askari hujiapisha kupoteza maisha kwa ajili ya Sultani na Bey. Hivi sasa baada ya hukumu ya mahakama inayomtaka kulipa mabilioni ya fedha; kuwalipa Benard Membe, Fatma Karume na Profesa Anna Tibaijuka, wako washangiliaji lakini wako pia wanaomhurumia.

Mabilioni hayo ni mengi kwa kijana kama huyu kuweza kuyalipa huku akijulikana kutokuwa na ukwasi wa aina hiyo. Nini kinafuata? Bila shaka katika taratibu za kimahakama zinazowapa walalamikaji fursa ya kukazia hukumu, ni majanga.

Hivi sasa wameibuka waliodai kuchafuliwa naye, wakiwamo Nape Nnauye, Yusufu Makamba na Zitto Kabwe. Pamoja na kumshukuru Mungu kwa uamuzi wa mahakama, sasa wanataka waliokuwa nyuma ya Musiba waibuke waseme nao ni upi upande wao. Ni yale yale ya mwana umleavyo ndivyo akuavyo. Musiba alilelewa hivyo- kuchafua watu kulikothibitishwa na mahakama ambako hakukukemewa enzi hizo, pengine angeacha na kuwapa uhuru wa kupumua aliokuwa akiwananga na kuwachafua!

He, kumbe ni yale yale kama ya Lengai ole Sabaya, ambaye tayari ni mfungwa baada ya mahakama kukubaliana na upande wa Jamhuri kuwa alichokifanya akiwa Disii wa Hai hakikustahili, hivyo kustahili tu kifungo cha miaka 30 gerezani.

Haya yote yaliyotokea kupitia mahakama zetu nchini, bila shaka yanatufungua macho kuona ni nini kibaya kinachoweza kuzuiwa na kusikia ni nini kibaya kinachoweza kuachwa kuzungumzwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Watanzania tunaweza kujifunza kupitia matukio haya pengine na mengine ambayo yako njiani kuibuka katika mahakama hizi hizi. Tena bahati mbaya sana, yanafanywa au yakifanywa na vijana na wakalindana mpaka sasa walikuwa na hatamu, ndio sasa mahakama zimewashushia marungu.

Kama Sabaya na Musiba wangezingatia kuwa kuna leo na kesho, wakaona umuhimu wa utawala bora na kuuheshimu, leo tusingekuwa tunashangilia au kusikitika kwa yaliyoamuliwa na Mahakama.

Je, sasa waliokuwa nyuma ya vijana wetu hawa, wako tayari kutoka mbele na kutoa ushuhuda wao na hata kuomba radhi kwa kuwasukuma kufanya waliyofanya na kuumiza watu kimwili na kiakili?

Kama wako tayari hawajachelewa na ndiyo sababu wanaombwa kusimama hadharani na kuuambia umma wa Watanzania waliokuwa wakiumia kupitia kauli za Mwanaharakati Huru na vitendo vya Jenerali Sabaya. Tunashndwa nini? Mbona majirani Rwanda walifanikiwa kupitia Gacaca? Watamke neno ili wasamehewe duniani na ahera, kwa kuwa hujafa hujaumbika!

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Ndugai kukopa si dhambi hata nchi zilizoendelea pia zinakopa



**Na Thobias Mwanakatwe**

WIKI hii Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliibua mjadala mzito baada ya kudai kuwa iko siku nchi inaweza 'kupigwa mnada' kutokana na madeni yatokanayo na mikopo.

"Juzi Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) ameenda kukopa Sh. trilioni 1.3. Sisi Watanzania wa miaka 60 ya uhuru kuzidi kukopa na madeni au tubanane banane hapa hapa, tujenge wenyewe bila madeni haya makubwa makubwa haya yasiyoeleweka. Ni lini sisi tutafanya wenyewe 'and how' (na kwa vipi)," alikaririwa akisema.

Aliongeza kuwa: "Tutembeze bakuli ndiyo heshima, tukishakopa tunapiga makofi, sisi wa kukopa kila siku!... tukasema pitisha tozo anayetaka asiyetaka pitisha tozo, lazima tuanze kujenga wenyewe, nani atatufanyia, yuko wapi huyo mjomba, tukapitisha."

Katika hali inayoonyesha ni kumjibu Ndugai, Rais Samia akaibuka Desemba 28 katika hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) Ikulu, Dar es Salaam, na kusema Serikali itaendelea kukopa ili kukamilisha ujenzi wa reli hiyo.

Akasema mkataba huo ulilenga kukamilisha kipande cha tatu kutoka Makutupora hadi Tabora chenye urefu wa kilometa 368, kitakachogharimu dola za Kimarekani dola bilioni 1.908 sawa Sh. trilioni 4.41 kati ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Yapi Merkez kutoka Uturuki.

Kutokana na kauli hiyo ya Ndugai, kuliibuka mijadala kwenye mitandao ya kijamii huku wengine wakisema hiyo ni ishara ya mtifuano mkubwa wa hoja zitokanazo na mitazamo juu ya namna bora ya uendeshaji wa nchi, njia za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, makundi ya kisiasa kushika hatamu ndani ya chama tawala, mtikisiko wa siasa za kistaarabu zilizoanza kutamalaki na mwanzo na kuharibu taswira ya nchi kimataifa.

Namshangaa Ndugai na kwa nini ameyasema haya mambo ya kukinzana na serikali ya awamu ya sita kwani wakati wa serikali ya awamu ya tano alikaa kimya. Nadhani hapa kuna jambo limejificha nyuma ya pazia.

Spika Ndugai afahamu kuwa kukopa si dhambi jambo la msingi unakopa kwa sababu gani? Ni lazima mkopo utumike kuboresha maisha na mazingira mazuri kwa ukuaji wa uchumi, hivyo tunakopa tukiwa na lengo la kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati itakayoleta tija na ukuaji wa uchumi. Lazima tutambue kuwa kwa kutegemea fedha zetu za ndani pekee, tutachelewa kwa sababu tunayo miradi mingi ambayo yote ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Pamoja na miradi ya ujenzi, kuna sekta za huduma pamoja na ajira na yote yanakwenda sambamba. Tusipokopa kwa sasa itatulazimu kukaa miaka mingine mitano bila kutoa ajira au kutoa ajira kwa uchache, kutokupandisha madaraja na mishahara kwa watumishi kwani miradi ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi.

Jambo la msingi la kutambua ni kuwa tunakopa fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kimkakati hasa wa reli ya kisasa ambayo baadaye itafungua nchi yetu na bandari za Tanzania kutumika kwa asilimia kubwa na majirani zetu ambao wataunganishwa na reli hiyo pamoja na kufungua biashara na Tanzania kuwa kitovu cha uchumi kwa ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika.

Kwa Tanzania bado deni letu ni himilivu kutokana na ukuaji wa uchumi. Ili kuwe na maendeleo ya kweli ni lazima sekta zoteziguswe kwa kuwa nchi ni zaidi ya ujenzi na miundombinu na kwa uchache tunazo sekta kama elimu, afya, kilimo, maji, mazingira, uvuvi na nishati.

Lakini pia uhusiano wa kimataifa zikiwamo balozi zetu kwenye mataifa mengine, hivyo ni lazima maendeleo yaguse sekta zote. Pia tutambue kwamba hiki ni kipindi ambacho uchumi wa nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania, umeyumba kutokana na UVIKO- 19.

Kuna kipindi nilishatoa tahadhari kwa viongozi vigeugeu kwamba ni hatari kwa taifa.

Niliyasema hayo baada ya Ndugai kuibua suala la ujenzi wa bandari ya Bagamoyo akisema serikali iangalie upya mradi huo iwapo ni jambo jema waendelee nao kwa madai kuwa Rais Hatari John Magufuli alishauriwa vibaya.

Kauli hiyo ya Ndugai ilipata mashambulizi mengi kwenye majukwaa mbalimbali watu wakihoji kwa nini alikaa kimya na kuishia kuunga mkono uamuzi wa serikali wa kusitisha ujenzi huo huku akitanabahisha kuwa mradi huo ulikuwa na kitapeli kabla ya kugeuka na kutoa kauli hiyo.

Ninavyokumbuka kipindi kile katika suala la bandari hiyo ni kwamba serikali haikufurahishwa na masharti ya China Merchants kuanzia mwaka 2014 na kuvutana nao hadi kipindi cha JPM ambaye hakutaka kupoteza muda zaidi. Aliwaambia China Merchants mwaka 2018 "STOP" kutokana na masharti magumu yaliyoelekea kuiweka nchi rehani kiuchumi na kisiasa.

Mwisho niseme tumwache Mama ajenge nchi kwani suala la kukopa hatujaanza sasa. Hata baadhi ya miradi mikubwa inayoendelea inaendeshwa kwa mikopo yenye masharti nafuu .

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# ATHARI ZA MIGOGORO YA NDOA KWA WATOTO KABLA NA BAADA YA KUZALIWA -2



**Na Mch.Dk. Enock Mlyuka**

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, tulizungumzia athari zinazotokana na migogoro ya ndoa kwa watoto huku ikibainishwa kwamba ndoa na familia ni kitalu na shule ya kwanza ya malezi na makuzi ya mtoto. Pia tabia na mienendo inajengwa katika familia.

Kwa mujibu wa wanasaikolojia, zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Kwa maneno mengine, wewe na mimi tulivyo leo ni zao la utoto wetu. Mtoto mwenye malezi mabaya ni mzigo wa baba na mama yake sasa na baadaye.

Pia ilitanabahishwa kwamba katika ulimwengu wa leo kumekuwa na wimbi la migogoro mingi ya ndoa na kuvunjika kwa ndoa nyingi na kwamba kwa baadhi ya familia, ndoa zimegeuka kuwa jela ya nyumbani na kusababisha upotoshwaji mkubwa juu ya kusudi na maana halisi ya ndoa na familia.

Sambamba na hilo, migogoro ya ndoa huondoa hisia za mapenzi na mvuto, hivyo kuchangia uwapo wa vitendo vya ukatili ndani ya ndoa na vifo. Migogoro ya ndoa huathiri afya na ustawi wa familia. Athari hizi haziwahusu wanandoa tu, bali wazazi ambako wanandoa hao wanatoka pia.

Athari za migogoro ya ndoa ni kubwa zaidi kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani huathiri sana makuzi na kusababisha msongo wa mawazo yenye athari mbaya (stress-leading to negative effects) kama inavyoelezwa katika sehemu zinazofuata.

Migogoro ya ndoa na kuvunjika ni mbegu ya uharibifu kwa watoto kwa kuwa inawabomoa badala ya kuwajenga. Migogoro ya ndoa huleta athari za kisaikolojia na kibailojia kama ilivyoelezwa wiki iliyopita.

Katika sehemu ya pili na ya mwisho, tunajadili athari zingine za migogoro ya ndoa kwa watoto katika umri mdogo katika maeneo yafuatayo;-

**Kitabia, kiroho na kijamii**

Migogoro ya ndoa huchangia katika kuharibu tabia na mienendo ya watoto. Watoto wanakuwa na maswali mengi yasiyo na majawabu kuhusu wazazi wao na hatima ya maisha yao. Watoto wengine wamemchukia hata Mungu kwa sababu wanaona amewakosea kwa kuwapa wazazi wa hovyo.

Hali hii huondoa ulinzi na usalama kwa watoto. Migogoro ya ndoa husababisha watoto kukosa uangalizi mzuri wa wazazi kiasi cha kuwafanya watoto kuwachukia wazazi wao na kutokupenda nyumbani kwao.

Matokeo ya hali hii ni ndoa, ajira na mimba za ututoni. Hatua hiyo inasababisha kutengenezwa kizazi kisicho na nidhamu, kutokuheshimu na kutokujali watu wengine hivyo kupelekea ongezeko la mmomonyoko mkubwa wa maadili na watu wakatili katika familia na jamii.

Baadhi ya watoto hujiingiza katika vitendo viovu kama vile ulevi, umalaya, ubakaji na ulawiti, wizi na uporaji wa mali za watu wengine wakiamini kuwa ni sehemu ya kukabili changamoto zao.

Kijamii, migogoro ya ndoa huzaa unyanyapaa (stigmatization) au hali ya kukataliwa na jamii. Watu wengi wakifahamu kuwa wazazi fulani ni wakorofi na watu wa migogoro au wenye tabia za hovyo, huzikataa familia hizo na kuzuia watoto wao kutokuoa au kuolewa au kushirikiana na watu kutoka katika familia hizo ili wasiwe kwazo na tatizo kwa watoto wao ambao wanaamini wamewalea vizuri, kwani hakuna mzazi mwenye akili timamu anayependa watoto wake wapate matatizo au kuvurugwa.

**Nini kifanyike?**

Kuwa baba na mama ni jukumu la heshima. Kila mzazi afahamu kuwa, katika kutekeleza jukumu la malezi kwa watoto wake anawajibika kwa Mungu aliyempatia watoto alionao. Kwa hiyo wazazi wasiwakoseshe watoto wao.

Wazazi wanaojitambua huruhusu watoto wao kujifunza mambo mema kutoka kwao. Malezi yao bora huwakuza watoto katika hali salama, ambayo itawawezesha kujisimamia katika maisha yao na kufanyika baraka kwao wenyewe, familia na jamii kwa ujumla.

Watoto waliolelewa vibaya hawako salama sana kwa kuwa ni rahisi kusombwa na chochote kitakachopita mbele yao kwa kuwa dhamiri zao zinakuwa butu kukabiliana na changamoto na mazingira tofauti. Mtoto mwenye malezi mabaya ni mzigo wa baba na mama yake.

Wanandoa wanapaswa kujifunza namna ya kusimama katika nafasi zao ipasavyo na kujiepusha kutengeneza mazingira ya migogoro isiyo ya lazima ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza katika maisha yao na makuzi ya watoto wao.

Vijana wasikurupuke na kuivamia ndoa pasipo ufahamu wa kutosha kuhusu taasisi ya ndoa na wale wanaotazamia kuoa au kuolewa nao. Ni muhimu kufahamu mambo ya msingi kuhusu mtu anayetarajiwa kuwa mume au mke kwani si kila mtu ana sifa za kuwa mke au mume wa mtu. Ni muhimu kufahamu familia anayotoka na mfumo wake wa maisha.

Pamoja na mambo mengine, umefika wakati sasa watu waone umuhimu wa kupima afya ya akili zao kabla ya kuingia katika ndoa ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima mapema. Kuruhusu mtu asiye sahihi katika maisha yako ni kuruhusu maumivu na kifo cha mapema. Mungu akusaidie!

■ **Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JANUARI 2, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13

**Shuhudia midemko ya kanga, vitenge**



**MAISHA NI NYUMBA**

Fanya uchaguzi wa malighafi sahihi kwa ujenzi wa nyumba



**HARUSI**

Ukurasa 12





**KOPE ZILIZOJAA**


# Mafuta nyonyo, alovela yatakupa furaha

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA









## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BEI, ANA, TENGA, KWETU, TWANGA, KWENYE




Alichokifanya daktari

MTOTO John aliambatana na baba yake kwenda madukani kwa ajili ya kununua nguo ya sikukuu. Walipofika eneo la maduka John alionekana kuhangaishwa na nguo nzuri zilizokuwa dukani.

Wakati akitupa macho huku na kule, mara alimuona mzee mmoja singasinga akiwa anachagua kanzu za kuvaa.

**John,** alizidi kumuangalia huku akiwa na wasiwasi mwingi na kumfanya baba yake amuulize.

**Baba:** John mbona una wasiwasi, kuna nini?

**John:** Namuonea huruma yule baba singasinga kwani anaweza kupata tatizo

Baba tatizo gani?

**John:** Mwalimu wetu alituambia eti Baniani mbaya, kiatu chake dawa ni kweli baba?

**Baba:** Sio kweli mwanangu, huo ni msemo tu unaomaanisha kwamba hata kama mtu ni mbaya, kuna vitu amevifanya ambavyo vimewasaidia watu

**SWALI**

Ndege aina ya popo wanaleta faida gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Je, unaishi maisha unayoyataka?

***KARIBU tena msomaji wangu tuanze mwaka 2022 kwa ushindi mkubwa. Tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kutupatia kibali kingine kuuona mwaka huu. Naye anatarajia tutatenda yote mazuri aliyoweka mbele yetu.***

Kumbuka maisha ni safari ndefu na umakini mkubwa unahitajika ili tuvuke salama. Yatupasa kujiweka wakfu kwa Mungu ili tuweze kufanya yale ambayo mbingu inataka tufanye kukamilisha kusudi la kuishi duniani humu.

Kuwekwa wakfu maana yake ni kuwa mali ya...Inaweza ikawa mali ya Mungu au mali ya mizimu ya kwenu. Mungu alikuumba kwa ajili ya kazi yake maalumu. Pamoja na ukweli huo, wapo watu wanaishi kinyume na matumizi ya mbingu inavyotaka.

Kuwekwa wakfu pia ni kupewa matumizi maalumu. Vile vile ni kuunganishwa kwenye chanzo fulani katika ulimwengu wa roho. Wapo watu wameunganishwa kupitia mizimu na madhabahu za kichawi.

Watu wengi wameunganishwa kupitia vyakula na kujikuta wanatumikia madhabahu za ufalme wa giza. Matokeo yake leo wamenaswa, wanashindwa kutoka.

> **Wengine wameunganishwa kupitia jina. Kama umebeba jina la babu au bibi yako, yale waliyokuwa wanapitia katika uhai wao, yaweza kukupata hata wewe.**

Vipo vitu vinawatokea watu katika maisha yao ya kila siku lakini wanashindwa kuzuia, Hawana nguvu ya kuzuia kwa sababu waliunganishwa na nguvu za giza, hivyo kuwawia vigumu.

Watu wengi wanachukuliwa na kupelekwa wasikotaka. Kujinasua katika hiyo mitego wanataka lakini hawawezi. Mfano dada au mama mwenye ndoa yake nzuri, lakini wanaomtamani nje ya ndoa ni waume za watu.Hii ni hatari sana!

Yeye ataona ni fahari kupendwa na waume za watu, au bosi ofisini, kumbe taratibu anajiondoa kwenye ndoa yake. Mahusiano ya aina hii huweza kupamba moto na hatimaye ndoa nzuri kuvunjika kirahisi.

Kuna makabila hadi leo yamejiunganisha kwenye miungu na bado yanafanya matambiko. Mungu alishaweka mapema kwenye amri zake kwamba tusiabudu miungu mingine ila Yeye.

Wako watu ambao leo kila wanalofanya haliendi, hata kama watainuka kiuchumi baada ya muda wanaporomoka. Kumbe chanzo ni maagano ya miungu ya kwao inafanya kazi kwenye maisha yao.

Kule ulikounganishwa ndicho chanzo cha matatizo yanayokusibu leo katika maisha yako. Utaona mtu ghafla anakuwa mlevi wa kupindukia, kumbe upo mnyororo wa roho ya ulevi kwenye familia husika.

Wengine wameunganishwa kupitia jina. Kama umebeba jina la babu au bibi yako, yale waliyokuwa wanapitia katika uhai wao, yaweza kukupata hata wewe.

Kama wazee hao walikuwa wacha Mungu, nawe utakuwa vivyo hivyo. Kama walikuwa washirikina nawe pia utaunganishwa. Kama ni wasomi, nyota ya elimu itaendelea kung'aa kwenye familia yenu. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Wazazi wengine wamewaita watoto wao majina ambayo yamewaletea madhara mabaya kimaisha. Mfano mtoto anaitwa Sikitu. Huyu katika maisha yake atakuwa wa kuhangaika, ataishi kwa kubangaiza na kila akipata hakikai, kila wakati hana kitu cha kuonyesha wenzake. Chanzo jina alilobeba!

Ni muhimu sana tunapojikuta njiapanda, turudi nyuma kutafuta chanzo cha matatizo yetu. Tusipofanya hivyo hatuwezi kupata ufumbuzi wa kudumu.

Kama nilivyojaribu kuainisha hapo awali kwamba chanzo cha matatizo ya watu wengi ni kujiweka wakfu kupitia nguvu za giza, madhabahu za mizimu badala ya kujiweka wakfu kwa Mungu.

Wengi wanaoteseka leo walijiweka au waliwekwa wakfu kwenye madhabahu za ukoo au mizimu. Wengi walikuwa matajiri lakini kwa sababu waliweka agano kwa shetani, leo wameporomoka, wanashangaa.

Kumbe walitumia utajiri wao vibaya kwa kutambikia miungu mingine ya kigeni, na kwa kufanya hivyo walimkabidhi shetani utajiri wao wote wa vizazi vyao. Yaani waliamini kuwa shetani anaweza kulinda mali zao wakasahau ulinzi watoka kwa Mungu aliye juu.

Ili watu wa aina hii wapone, ni muhimu kumrudia Mungu, kwanza kwa kuvunja agano na shetani, kisha kuweka agano jipya na Mungu wa mbinguni. Kwa kufanya hivyo, maisha yako yatakuwa salama na utafanya yale yote mazuri ambayo mbingu inataka uyafanye.

***Hadi wiki ijayo. Je, una maoni au kisa ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Heri ya Mwaka Mpya 2022, tujipange kutimiza malengo

MWAKA 2022 umeanza, hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa afya, amani na alivyotuwezesha kuyafikia malengo tuliyokuwa tumejiwekea mwaka 2021. Hata kama hayakufikiwa, bado tunafundishwa kushukuru kwa kuwa kwenye kushukuru kuna ushindi.

Watanzania tuna sababu nyingi za kumshukuru Mungu kwa kuwa amani iliyopo ni jambo kubwa ambalo wengine wanalilia kila siku na wako ambao walisitisha mapigano kusherehekea mwaka mpya na sasa watarudi kuendelea.

Mwaka 2021 kama ulivyokuwa 2020, ulijawa na hofu kubwa hasa kutokana na janga la UVIKO-19 ambalo hadi sasa linaisumbua dunia. Nasi Tanzania tuliathirika kwa kiasi kikubwa na janga hilo.

Athari za UVIKO-19 zimeonekana kwenye uchumi kwa kuwa sekta nyingi ziliumia hasa utalii ambayo hutegemea watu kusafiri kutoka eneo moja kwenda lingine. Kutokana na ugonjwa huo ambao unaambukizwa kwa kasi wengi walishindwa.

Tunaanza mwaka 2022 UVIKO-19 ikiwamo na tunaishi nayo huku wataalamu wakitueleza kuwa tutaendelea kuwa nayo maisha yetu yote bali kinachotakiwa ni kuhakikisha tumechanja na kuchukua hatua zote muhimu.

Tunapaswa kuendelea kujilinda ili tuyafikie malengo tunayojiwekea ya mwaka 2022 kwa kuwa ili tuyafikie ni lazima kuwa na afya njema ambayo ndiyo msingi, hivyo lazima tuchanje ili kuimarisha kinga ya mwili, kula vyakula vinavyotusaidia na kuchukua tahadhari muhimu.

Kwa siku hizi za mwanzo wa mwaka, ni wakati wa kuweka malengo ambayo lazima kuyawekea mikakati ya kutimiza ili tutakapouaga mwaka huu iwe kufanya tathmini ya namna tulivyofanikiwa kutekeleza na vikwazo vilivyopo.

Ikiwa kila mmoja atafikiri namna ya kufikia malengo yake, basi kuna uwezekano mkubwa wa kubadili maisha ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kwa kuwa mabadiliko ya kiuchumi kwa mtu hata kama anakua ni faida kwa nchi kwa kuwa sasa watakusanya kodi ambayo itakwenda kwenye huduma za kijamii kama elimu, afya, maji na miundombinu.

Tunapouanza mwaka 2022 lazima tuhubiri umoja wa kitaifa ili tuendelee kuwa na amani. Bila umoja huo, huenda tukabaki kuwa vipande vipande ambavyo vitatufikidha kwenye mkwamo.

Ni lazima waliopewa mamlaka kuwajibika kwa wananchi ambao wamewapa nafasi hizo na wanawalipa mshahara na marupurupu mengine, kwamba sasa tuone mabadiliko makubwa kwenye sekta mbalimbali na si utendaji kazi wa mazoea.

Maeneo ambayo wananchi huyakimbilia kila siku kupata huduma ni mahakamani, hospitalini, polisi na ofisi mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, ni matarajio kuwa mwaka 2022 hautakuwa na utendaji kazi wa kimazoea ambao umeanza kujitokeza kwa watendaji kuwa mabosi badala ya watumishi wa watu.

Vyombo vya kutoa haki visimamie haki kwa kuwa amani iliyopo inawategemea sana. Haki ya mtu ikiminywa atatunza maumivu moyoni kwa muda Fulani lakini kuna wakati atashindwa kuvumilia.

Kwa polisi mwaka 2021 wananchi wengi wengi walipaza sauti dhidi ya uonevu uliopo kiasi cha Rais Samia Suluhu Hassan kuzungumza mara mbili juu ya hilo, akiwataka kubadilika na kuacha kuonea raia.

Sasa tuone mabadiliko kwamba watu wasibambikiwe kesi utendaji kazi wa uadilifu kwa kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake,ili isiwe ni sehemu ya kuumiza watu na siyo salama au haki.

Rangi ya blue bahari inayopakwa kwenye vituo vya polisi ina maana ya haki, sasa isiwe kinyume chake. Haki itendeke na ionekane kutendeka ili kuondoa malalamiko na kutokuaminiana.

Hivi karibuni, Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, IGP Simon Sirro, alieleza kuwa uhalifu umepungua kutokana na ushirikiano mkubwa baina ya wananchi na polisu, huku akiomba ushirikiano huo uendelee ili kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Ushirikiano wa wananchi utazidi ikiwa wataona haki inatendeka kwa kuondoa vitendo vyovyote visivyofaa,kwamba vituo vya polisi visigeuke kuwa Mahakama,Magereza bali watu wapelekwe mbele ya mkono wa sheria kwa hatua zaidi.

Pamoja na hayo yote, bado Nawaza kwa Sauti inatambua na kuthamini mchango wa Jeshi la Polisi kwa nchi, wanastahili pongezi kwa kuwa miongoni mwao wapo waadilifu na ambao siyo wanatimiza usemi wa kwenye msafara wa mamba na kenge wapo.

***Mungu Ibariki Tanzania.***

# HARUSI



Desemba 12, 2021, ilikuwa ya furaha kwa Mordecai Mleke baada ya kufunga ndoa na Faines Khalfan katika kanisa la TAG Ubungo na kufuatiwa na sherehe ya kipekee iliyofanyika Ukumbi wa Kristu Mfalme, Tabata jijini Dar es Salaam.











# MITINDO

## MWAKA WA MITINDO

# Shuhudia midemko ya kanga, vitenge

MWAKA 2022 umeingia kukiwa na heka-heka ya kukabiliana na ugonjwa wa corona ambao unazidi kuitikisa dunia

Pamoja na watu kuwa na hofu na mashaka kuhusu ugonjwa huo, lakini hawawezi kusahau suala zima la mavazi kwani hilo ni jambo muhimu katika maisha ya kila siku.

Mwaka 2021 ulikuwa na mafanikio katika sekta ya mitindo, licha ya masharti ya kupambana na corona kuathiri mtiririko mzima wa masoko na ubunifu wa mavazi.

Baadhi ya wabunifu wa hapa nchini, wameukaribisha mwaka mpya kwa kutabiri kwamba utakuwa wa neema kwao kutokana na watu wengi kuhitaji mavazi ya kisasa zaidi.

Mustafa Assanali mbunifu na mwandaaji wa jukwaa la Swahili fashion, amesema wanatarajia kuwa na mabadiliko zaidi hasa kutokana na vikwazo vingi kuondolewa.


"Mwaka jana kulikuwa na vikwazo vingi hasa nje ya nchi na kusababisha baadhi ya malighafi kuwa juu, lakini mwaka huu natarajia mambo yatabadilika na kuwa mazuri zaidi," amesema.

Amesema bado mavazi ya kiafrika hasa khanga, vitenge na mabazee yatazidi kung'ara na kama wabunifu wataongeza vionjo, basi nguo hizo zitakuwa hazishikiki katika soko.

"Mwaka jana tumeanza kuliweka soko vizuri hasa katika mavazi ya kiafrika, natumaini juhudi hizo zitaendelea na kufanya soko kuwa zuri na wahitaji kuongezeka zaidi," ameongeza kusema.








UREMBO







KOPE ZILIZOJAA

# Mafuta nyonyo, alovela yatakupa furaha

KOPE ni moja ya kiungo muhimu katika kung'arisha sura, kutokana na umuhimu wake wanawake wamekuwa na njia nyingi katika kuziboresha.

Uwekaji wa kope bandia ni njia moja ya uboreshaji wa kuongeza ukubwa wa nyusi ili mwonekano uwe wa kupendeza zaidi.

Lakini katika uwekaji wa kope bandia unatakiwa uwe wa uangalifu, kwani inapokaa muda mrefu unaweza kupoteza hata zile chache ulizokuwa nazo mwanzoni. Wanawake wengi wamekuwa wakikesha kwenye saluni za kubandika kope ili kubadilisha mwonekano wao.

Hata hivyo, kuna njia za asili unaweza kumaliza tatizo la kuwa na kope chache na kuondokana na matumizi makubwa ya pesa kwa ajili ya kupata huduma ya kubandika kope.

Nitakuonyesha jinsi ya kupata kope nzuri zilizojaa kama mtu aliyebandika kwa kutumia mafuta ya Mnyonyo, Alovela na Vitamin E.

**Mahitaji**

Chukua brashi ya kupakia mascara, mafuta ya mnyonyo kiasi unachotaka, ute wa Aloe Vera na Vitamin E.

**Jinsi ya kutumia**

Chukua vitu vyote vichanganye kwa pamoja baada ya hapo chukua brashi ya kupakia chovya kwenye mchanganyiko wa vitu vyako, kisha paka kwenye mzunguko wa kope juu na chini.

Paka kila siku usiku baada ya mwezi utaona matokeo mazuri kwa sababu kope zako zitakuwa ndefu na zitakuwa ngumu si rahisi kuona zinanyofoka nyofoka hovyo.

Njia nyingine ni kutumia mafuta ya mgando ya Vaseline ukiwa unapaka kila siku kwenye kope zako zinasaidia kurefusha, kujaa na kuwa na mvuto zaidi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Punguza mwili kwa vyakula hivi....

WAKATI watu wapo katika likizo ndefu ya msimu wa Sikukuu ya X-Mas na Mwaka Mpya, hali inaweza kuwa tofauti pale inapofika ukingoni kwa baadhi kuongezeka mwili na kupoteza mwonekano wao wa asili.

Hata hivyo, usiwe na hofu sana kwani unaweza kupunguza uzito wako kwa siku chache kama utafuata njia sahihi ya kuondoa unene.

Kama unaona mwili wako umeongezeka kwa haraka, unaweza kupunguza mwili na kurudi katika hali yako ya zamani kwa kula vyakula vifuatavyo.

**MAYAI**

Mayai yana Protini nyingi sana ambazo zinamtosha kifaranga kutoka ndani ya yai kuishi vizuri.

Utafiti unaonyesha binadamu wa kawaida anatakiwa ale mayai angalau matatu kwa siku kuondoa uwezekano wa kuongeza cholestro ambazo ni hatari kwa moyo.

Ukiamka asubuhi ukala mayai



kama sehemu ya kifungua kinywa chako unaweza kukaa muda mrefu bila njaa.

Mayai nayozungumzia hapa ni yale anayotaga kuku mwenyewe hasa ya kienyeji.

**MBOGA ZA MAJANI**

Mboga hizo ni kama mchicha, bamia, nyanya chungu, kabichi, spinachi, kisamvu, msusa na zingine.

Zina vitamini nyingi, fibres au nyuzi nyingi na wanga kidogo hivyo zinaweza kuliwa kwa kiasi kukubwa na kujaza tumbo bila kusababisha unene lakini pia zinaitwa kitaalamu kama antioxidant yaani zinaweza kuondoa sumu mwilini.

**SAMAKI**

Samaki wana kiasi kidogo sana cha mafuta, wana protein nyingi ambayo itakuacha muda mrefu ukiwa umeshiba na kukufanya usile sana.

Lakini pia samaki wana kemikali ya omega 3 ambayo ni muhimu sana kwenye mwili kwani huzuia magonjwa ya moyo na kusaidia kazi ya kuchoma mafuta.

**MAHARAGE**

Maharage ni chakula kizuri sana cha asili ambacho kimewakuza watu wengi, kina protini ya kutosha pamoja na fibre yaani nyuzi ambazo ni muhimu sana.

**MAPARACHICHI**

Maparachichi yana sukari nyingi, yana mafuta na nyuzi ambazo ni muhimu sana kwa afya ya moyo na kupunguza uzito.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Fanya uchaguzi wa malighafi sahihi kwa ujenzi wa nyumba

UKUTA wa nyumba ni sehemu muhimu na ya kudumu na ndiyo hushikilia ustawi na uimara wa kwenye nyumba au jengo lolote.

Mara nyingine matokeo ya nyumba nzuri na uimara wake, huonekana kwa nje ikiwa imenakshiwa vizuri bila kujua siri ya vitu gani vilivyotumika mpaka kufikia kuonekana katika hali hiyo.

Mtaalamu wa ujenzi, Victor Mkalama, anasema ukuta anaozungumzia ni ule ambao hutokana na mchanganyiko wa zege au mawe na kufanyiwa utaalamu wa uashi na kusimama kama ukuta ambao baadaye huitwa nyumba.

Anasema jambo la msingi la kufahamu katika kutambua kama unataka kuwa na ukuta wa nyumba bora, imara na wa kudumu ni kuhakikisha unakuwa makini na aina ya malighafi unayotumia ambayo inaendana na mazingira ya eneo husika.

Jambo lingine anasema la kuzingatia ni mtindo na muundo wa nyumba husika.

"Katika hili unapaswa kufahamu pia kwamba nyumba unayojenga ni ya mtindo na ya muundo gani na pia kama ni ya kutumia mawe au tofali ili fundi anayejenga akushauri kutokana na mazingira ya eneo lako," anasema Mkalama.

"Ukuta bora, imara na ambao ni wa kudumu unategemea sana na aina ya malighafi. Ikumbukwe kwamba ukuta wa tope, mawe au tofali ubora na uimara wake hutofautiana sana ndiyo maana tunashauri sana kupata ushauri kutoka kwa wataalamu.



"Kwa hiyo hata katika ufundi katika kujenga nyumba yenye ukuta bora hakuwezi kutokana na ubunifu pekee kutoka kwa fundi, inategemeana sana na hivyo vitu vitatu ambavyo ni malighafi, mazingira ya eneo ambalo nyumba husika inajengwa na muundo wake, halafu ufundi ni wa mwisho," anasisitiza.

Pia anasema katika kazi ya kujenga ukuta wa nyumba au wa jengo lolote ni lazima kuzingatia uzito unaoendana na jengo husika.

"Ukuta usioendana na aina ya jengo unaweza kuleta shida kwenye jengo au nyumba baadae. Na aina ya kwanza ya ukuta unaobeba uzito wa jengo hujengwa kwa kutumia tofali za kuchoma, mawe au matofali ya zege au mchanga.

"Kazi ya ukuta wa aina hii hufanya kazi kubwa ya kuchukua na kusafirisha uzito wa paa au jengo hata kama ni nyumba ya kawaida au ghorofa," anasema.

## Namna ya kupamba taa za Krismasi nyumbani



NYUMBA nyingi wakati wa sherehe za Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya zinang'arishwa kwa taa mbalimbali za mapambo. Taa za rangi tofauti na angavu zinaleta mandhari nzuri na kuvutia kwenye macho ya watu.

Zifuatazo ni aina za mitindo ya kupamba nyumba kwa kutumia taa za Krismasi.

**1:** Soksi za tawi la mti wa krismasi ni aina nzuri ya kupamba nyumba yako na kuifanya kuwa na mwonekano wa kuvutia.


Unatakiwa kuweka tawi la mkrismasi ukutani na kisha kuning'iniza taa za rangi ambazo zikiwashwa zinaleta mvuto wa kipekee.

**2:** Muundo wa theluji ni mapambo yanayopendelewa na wengi, kwani ndani ya nyumba kunakuwa na taa nyeupe hafifu na mapambo mengine yanayofanana na theluji yanayoleta taswira nzuri zaidi.

**3:** Kupamba kwa mishumaa ya rangi nyekundu ni nzuri zaidi kwani inaleta mng'aro wa kiasili. Mwanga wa mishumaa na taa za rangi zinapokutana hutengeneza mwanga unaopendeza na kumfanya mtu kuwa na furaha.

**4:** Kupamba taa ya Krismasi ya dhahabu na mipira ya tausi ni moja ya mapambo yanayopendwa na wengi. Mipira ya Krismasi yenye rangi nyeupe na fedha inaonyesha vyema maandishi ya ujumbe, unashauriwa kuchukua yenye rangi ya kijani na nyekundu kwa kuwa ndiyo yenye mwonekano wa kuvutia.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA 2022
Na MUHIDINI MSAMBA
0758 122772
SMS
FULL KAUZU
MZAZI
HAKUNA CHA BANDU BANDU
MSIMU WA UKAMUAJI UMEFIKA
ADA ZA SHULE BINAFSI (ST EMMY)
TWAFWAAA...
MAKAVU MUBASHARA
UKINIKUBALI SIWEZI KUKUTELEKEZA
KWA SURA GANI ULIYONAYO
NIKUBALI MREMBO ILI ULE RAHA, MIMI NI PEDEJEE HAPA MJINI , YALE MAJENGO YA KARIAKOO NI YA UKOO WETU NA MIMI NDIYE MSIMAMIZI
UKIMALIZA KUMMIMINIA MASHAIRI YAKO MAIWAFU JIANDAE KUMIMINIWA MASHAIRI YANGU YALIYOENDA VIDATO
CHOMA
WENGINE MWAKA MPYA TUMEUPOKEA HIVI NAOGOPA KUTIA NENO NISIJE NIKAMWAGIWA MAHARAGE YA MOTO
MZUNGU WA NNE UNAKERA HAKI YA NANI, USIKIE KWA MWENZIO OMBA USIKUPATE
KILA NINAKO PITA WATU WANASHANGAA KITAMBI CHANGU
WENZIO WANAFANANISHA KITAMBI CHAKO NA MIEZI YA UJAMZITO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KIU YA MAJI HAIKATWI KWA MATE

## HABARI KIMATAIFA



Ulipuaji wa fataki katika daraja kuu la mjini Sydney nchini Australia ulipamba makaribisho ya Mwaka 2022 usiku wa Desemba 31 bila kuwa na umati wa watu. **PICHA: AP**

# Dunia ilivyokaribisha 2022 kimyakimya kuhofia corona

**LONDON,** UINGEREZA

DUNIA imeadhimisha Mwaka Mpya wa 2022, wakati mataifa mengi yameweka masharti ya kusherehekea kimyakimya kutokana na kupamba moto kwa janga la COVID-19.

Hata hivyo, baadhi ya nchi zimepuuza tahadhari za kuzuia maambukizo mapya.

Miji ya London nchini Uingereza na Paris Ufaransa ilipiga marufuku mikusanyiko ya watu na uwashaji fashifashi, huku Madrid nchini Hispania ikiagiza sherehe hizo kufanyika kwa kiwango cha wastani.

Mjini Berlin hakukuwa na fashifashi kwenye lango la Brandenburg kama ilivyozoeleka, ambapo maelfu kwa malaki ya watu hukusanyika.

Polisi katika mji mkuu huo wa Ujerumani waliwataka watu kutosogelea eneo hilo.

Katika mji wa Rome, nchini Italia polisi walifunga baadhi ya maeneo ya katikati ya mji huo kuzuia mikusanyiko ya watu.

Hata hivyo, nchini Urusi katika mji wa Moscow, licha ya baridi kali mamilioni ya watu walijitokeza mitaani kuuaga mwaka 2021 na kuukaribisha 2022, wakirusha fashifashi na serikali ikiondoa marufuku ya mikusanyiko.

Barani Asia, maadhimisho yalifanyika kwa tahadhari katika miji ya Beijing, Hong Kong, Jakarta na Bangkok.

Rais Xi Jinping wa China, alitumia hotuba yake ya Mwaka Mpya kuwataka wananchi wake kuweka mkakati na kuchukua tahadhari dhidi ya kitisho dhidi ya lengo la muda mrefu la Chama cha Kikomunisti la kuigeuza China kuwa taifa kubwa duniani.

Mjini Dubai, jengo refu kabisa duniani la Burj Khalifa, liliwasha mataa na mionzi huku fashifashi zikirushwa kuukaribisha mwaka 2022.

Nchini Afrika Kusini, taifa la kwanza kuripoti aina mpya ya kirusi cha corona ya Omicron, iliondoa marufuku ya kutotoka nje nyakati za usiku ili kuruhusu watu kusherehekea Mwaka Mpya.

Fursa kama hiyo hawakuipata watu wa Morocco, ambako marufuku dhidi ya mikusanyiko na sherehe iliendelea kama kawaida.

Nchini Marekani, jiji kubwa la New York lilirejea kwenye sherehe zake za kila mwaka katika Viwanja vya Times, licha ya maofisa wa afya kuonya dhidi ya mikusanyiko kama hiyo inayoweza kusambaza kwa haraka virusi vya corona.

Mamlaka za jiji hilo lenye watu wengi zaidi nchini humo zilisema kwamba zimedhibiti idadi ya watu wanaofurika kwenye sherehe kama hizo hadi kufikia 15,000 pekee.

Katika mji wa Rio de Janeiro nchini Brazil, kawaida huwaleta pamoja zaidi ya watu milioni tatu katika fukwe za Copacabana, ziliendelea kama kawaida.

Maadhimisho ya kwanza ya Mwaka Mpya yalianza kwa wakaazi wa visiwa vya Samoa na Kiribati kusini mwa bahari ya Pasifiki, na baadaye New Zealand.

BBC

# Askofu Tutu afanyiwa mazishi ya kitaifa

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

MAZISHI ya kitaifa ya mwanaharakati aliyepinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, Askofu Mkuu Desmond Tutu, yalifanyika jana na kuhudhuriwa na watu mbalimbali mashuhuri.

Katika tukio hilo, ibada ya wafu ilifanyika katika Kanisa Kuu mjini Cape Town, ambako pia majivu yake yatawekwa baada ya kuchomwa moto.

Tutu, ambaye ni mshindi wa tuzo ya amani ya nobel, alifariki dunia Jumapili iliyopita akiwa na umri wa miaka 90.

Kifo chake kiliibua majonzi miongoni mwa raia wa Afrika Kusini.

Maelfu ya watu wametoa heshima zao za mwisho katika Kanisa Kuu la St George's ambako mwili wake umekuwa ukilazwa katika jeneza la kawaida.

Askofu Tutu alikuwa mmoja wa watu waliokuwa na msukumo mkubwa nyuma ya vuguvugu la kumaliza sera ya ubaguzi wa rangi iliyotekelezwa na serikali ya wazungu wachache dhidi ya weusi walio wengi nchini Afrika Kusini kuanzia mwaka 1948 hadi 1991.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisoma wasifu wake mkuu katika mazishi hayo ya kitaifa ambako watu 100 pekee ndio waliohudhuria kwa sababu ya masharti ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Kiongozi huyo wa kidini aliyeheshimiwa alikuwa amesisitiza kuwa hapapaswi kuwa na matumizi ya majivuno au ya kifahari katika mazishi yake na alisema anataka kuzikwa katika jeneza la bei ya chini iwezekanavyo.

Alisema pia kwamba maua atakayopewa katika kanisa kuu yatatoka kwa familia yake pekee, kulingana na Wakfu wa Tutu IP Trust na the Desmond and Leah Tutu Legacy.

Majivu ya mwili wake yanatarajiwa kuwekwa nyuma ya madhabahu katika Kanisa Kuu la Anglikana la Mt. George mjini Cape Town, ambalo alilihudumia kama Askofu Mkuu kwa miaka 35.

Awali ilifichuliwa kuwa mwili wa Tutu utachomwa kwa kutumia mbinu ya maji inayofahamika kama 'aquamate' iliyoelezewa kama mbinu rafiki kwa mazingira kuliko kuuchoma kwa moto wa kawaida.

Watu wengi katika mji wa Cape Town walijitokeza kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa Askofu Tutu ambao ulilazwa ndani ya jeneza.

Mwanaume mmoja aliyeitwa,Wally Mdluli, aliyesafiri kwa baiskeli umbali wa kilomita zaidi ya 1,000 kutoka upande Bloemfontein hadi Cape Town, alielezea jinsi alivyoomba msaada kutoka kwa marafiki na familia wamsaidie kulipia safari yake na kulala kwenye kituo cha mafuta njiani.

"Nilihisi nimeridhika baada ya kuliona jeneza. Ni kama roho yake iko ndani yangu," alimwambia mwandishi wa BBC .

Askofu Tutu alitumia haiba na utambulisho wake kuzungumza wazi dhidi ya ubaguzi wa rangi na unyanyasaji wa watu weusi katika nchi yake, alisema hivyo kwa misingi ya kidini na siyo kisiasa.

Baada ya Nelson Mandela kuwa rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini mwaka 1994,Tutu aliteuliwa kuongoza tume ya ukweli na maridhiano iliyobuniwa kuchunguza uhalifu uliofanywa na wazungu na weusi wakati wa enzi ya ubaguzi wa rangi.

BBC

MAKALA

# UTAMADUNI HUU UTALIANGAMIZA TAIFA



Na Magabilo Masambu

KUELEKEA mwishoni mwa mwaka 2021, niseme machache yaliyojitokeza miaka michache ambayo tusipoyasema yatajenga utamaduni wa kudumu baadaye. Kwa kawaida, utamaduni huanza kujengeka taratibu pale tabia fulani zinapoanza kujitokeza. Zikiwa tabia njema basi hujenga utamaduni mzuri katika jamii lakini zikiwa mbaya hujenga utamaduni mbaya.

Kwa mila na desturi pamoja na utamaduni wetu wa Kiafrika hasa za kitanzania toka zamani, tumekuwa na utaratibu wa kuheshimiana lakini zaidi kuheshimu mawazo na maoni ya wale ama waliotutangulia kiumri au kimamlaka. Nakubali kwamba kutangulia huko hakuwezi kumfanya mtu akawa sahihi kwa kila jambo lakini angalau kwa uzoefu wa kuona na kujifunza mengi ama katika madaraka au maisha ya kawaida, waswahili wanasema kuishi kwingi kuona mengi.

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya viongozi hasa vijana kujitokeza waziwazi kuwakemea viongozi wastaafu au kutoa matamko yenye kuwatisha wazee wetu eti wasitumie uhuru wao wa kikatiba kutoa maoni mbalimbali kuhusu mambo mazito yanayoihusu nchi huku wakimwagiwa sifa kedekede kwa viongozi walioko madarakani.

Uhakika nilio nao ni kwamba wanaokusifu leo ukiwa na madaraka ya kuwateua kwenye nafasi mbalimbali ndio watakaokukemea utakapoyakosa madaraka hayo. Jambo moja muhimu ni kuwa makini sana na watu wanaokusifu leo na kuwakemea wengine kesho ama watakutukana au kukwambia umepitwa na wakati. Kwa hiyo ukae kimya kama ambavyo tumewahi kusikia kauli kama hizo kutoka kwa baadhi ya viongozi vijana kwa umri lakini pia kwa uzoefu katika eneo la uongozi na siasa. Jambo hili ni sawa kabisa na suala la kufuga joka nyumbani mwako ambalo kila siku unalipatia chakula siku, likikikosa ama litakutafuna mwenyewe au wanao. Hivyo ni kuwa makini sana na watu wa sampli hiyo na hasa wanaokwambia tuko nyuma yako. Kuna siku utageuka hutawaona. Tukiwafurahia leo wanapojaribu kuwakemea wazee wetu kesho tukistaafu wembe ni uleule tutakemewa na sisi.

Taifa lisiloheshimu mawazo ya wazee waliotangulia katika nafasi mbalimbali, litakosa mwelekeo mzuri kwa sababu ni vigumu kupata historia iliyo hai si ya kusoma kwenye vitabu. Tumefika mahali ambapo baadhi ya wazee wastaafu kwenye nafasi mbalimbali wamekuwa na hofu ya kutoa maoni yao. Wakati mwingine wanalazimika kukanusha yale wanayoyasema kwa hofu tu kwamba wataonekana wasaliti badala yake wanaamua kukaa kimya na pale yanapotokea matatizo ambayo yangeweza kutatuliwa na ushauri wao wanaishia kusema tulijua!

Viongozi wote wenye nafasi mbalimbali lazima tufahamu kwamba hizi nafasi tulizo nazo si za kwanza kwetu. Walishakuwepo watu kama sisi wakapita, hivyo pamoja na mapya tunayoyataka yafanyike ni muhimu sana kurejea yaliyopita ili kuona wenzetu walifanikiwa au kushindwa wapi ili tufanye marekebisho yenye tija kwa taifa . Hayo hayatawezekana kama tutaendelea kuwafanya waliopita washindwe kutoa ushauri wao waziwazi.

Miaka ile hasa katika awamu ya pili ya mzee wetu Ali Hassan Mwinyi, Mwlaimu Julius Nyerere akiwa amekwishastaafu na akiwa Butiama, alipokuwa anaona kuna jambo fulani halijakaa sawa, alikuwa anajitokeza waziwazi kusema hili hapana wakati mwingine aliendewa kuulizwa mzee hapa tunafanyaje? Utaratibu huo nadhani aliendelea nao mpaka mwisho wa maisha yake hapa duniani.

Wakati mwingine inaweza kuonekana kwamba wastaafu hawa wanaingilia masuala ambayo walishindwa kuyafanya bado huo hauwezi kuwa utetezi wa kupata fursa ya kutoa maoni yao. Inawezekana wakati wao changamoto wanazoziona leo hazikuwapo. Wengine wanasema kama wanataka kutoa maoni, uko utaratibu. Nakubaliana nalo lakini si kila maoni yafuate utaratibu huo. Hiyo itakuwa janja ya kuwapora uhuru wao wa kikatiba.

Tatizo linaweza kuwa si la wazee hawa pengine wanasubiri sana kuonwa kwa ajili ya ushauri. Hawaonwi, namaanisha wazee wengi hupenda kufuatwa kuulizwa baadhi ya mambo lakini nafikiri waulizaji hatuendi kuwauliza, hivyo tunajifanyia tu mambo yetu kwa kuamini kwamba tunazo akili nyingi na uzoefu wa kutosha jambo ambalo binafsi naona si kweli. Kwa hiyo wanapoona mambo ambayo wanafikiri wangeulizwa na hawajaulizwa wanaamua kuyasema hadharani.

Nadhani tukiwapa fursa si tu wazee wastaafu bali kila mtu akiwa na nafasi sawa katika utoaji wa maoni namna ambavyo sisi kama nchi tunataka kujiendesha mambo mengi maovu yataepukika. Jambo hili pia halitafanikiwa ikiwa hatutajiona kama ndugu na kwamba taifa letu ni moja na makusudi ya kila mtu ni kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa nchi yenye sifa njema duniani.

Mambo haya lazima tuyatafakari sana kama taifa inawezekana pameanza kuwa na tatizo kubwa kunzia kwenye familia zetu tabia ya kutowahesimu wazee wetu. Kuna wakati unasikiliza matamko mbalimbali ya baadhi ya viongozi unajiuliza hawa nao wana wazazi au wazee nyumbani kweli au wanafanya haya ili wale waliowapa nafasi hizi wafurahi. Unajiuliza tena hawa wanaosikiliza haya wanafurahi kweli na kama hawapendezwi mbona hawachukui hatua? Mwisho, nyumba yenye wazee ni nyumba yenye baraka. Walioafanikiwa kuishi na wazee wao watakuwa wananielewa. Kuna wakati wakiwapo huwa umuhimu wao hauonekani sana wanapoondoka ndipo unajua kwamba umekosa jambo muhimu sana.

Jambo hili ndilo huwa linafanya watu wengi kuyapamba makaburi kwa vigae vyenye thamani tusisubiri kuweka picha zao kwenye kuta za majumbani mwetu na kuzihifadhi vizuri tuwaheshimu na kuthamini michango yao ingali wakiwa hai ili kuipa nafuu mioyo yetu pindi tunapowakosa.

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wabongo watamkumbuka Defao kucheza tumbo wazi



Na Adam Fungamwango

KILIKUWA kishindo kikuu kilichKILIKUWA kishindo kikuu kilichotokea Jumatatu wiki hii zilipotolewa taarifa za kifo cha mwanamuziki maarufu wa muziki wa rhumba na Soukous Afrika na dunia nzima, Le General Defao.

Kwa Watanzania, ni mwanamuziki anayefahamika sana hasa kwa kizazi cha waliokuwa wazee, vijana na watoto kuanzia miaka ya 1990. Aliwachezesha Watanzania kwa nyimbo zake kali, zilizokuwa lazima zipigwe kwenye sherehe mbalimbali za harusi, kiserikali na kijamii.

Ni miaka ambayo ndiyo televisheni zilipokuwa zikiingia Tanzania na watu wachache sana walikuwa nazo. Ndio wakati watu wazima na watoto walikuwa wakijazana kwenye nyumba za watu waliokuwa nazo, pamoja na tamthilia na filamu. Pia kulikuwa na mikanda ya wanamuziki mbalimbali waliotamba kipindi hicho kama Pepe Kalle, Aurlus Mabele na kundi lake la Loketo, Soukous Stars ya kina Yondo Sister, Bozi Boziana, Kanda Bongoman pia Defao.

Kwenye video zake, Watanzania pamoja na nyimbo zake tamu, walimhusudu Defao kutokana na uwezo wake wa kucheza licha ya kuwa na umbile kubwa. Wakati mwingine alivua shati na kucheza tumbo wazi. Si kwamba alikuwa akicheza, mradi kucheza bali alikuwa na uwezo wa kucheza kwa staili yoyote ile, akiwa mwepesi kuliko umbile lake.

Alikuwa na uwezo wa kucheza kwa mbwembwe, kwa madaha na ustadi mkubwa kuliko wanamuziki wengi wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo. Sherehe yoyote ilikuwa haiwezi kumalizika bila kupiga nyimbo za Defao, halafu watu wakakuelewa.

Nyimbo kama 'Sala Noki', 'Nakusema Nikutaka', 'Madova', Kamille Kikuta' na 'Bibi Yangu Hanitaki Tena' zilivuma kama moto wa nyika na kumsababishia kuwa na mashabiki wengi pande mbalimbali za dunia, ikiwemo Tanzania ambako pamoja na kujizolea mashabiki wengi, alifanya ziara mara kadhaa.

Mwaka 2000 aliangua kilio, alipokuja nchini kufanya uzinduzi wa albamu yake mpya aliyoirekodi nchini Ufaransa, lakini aliikuta tayari ipo kwenye maduka nchini na inauzwa kama njugu.

Huyu jina lake kamili ni Defao Matumona. Defao aliyekuwa na umri wa miaka 62, alifariki dunia Jumatatu, Desemba 27, katika Hospitali ya Laquintinie huko Douala, Cameroon, ambako alikuwa amelazwa hospitali baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Defao alizaliwa Desemba 31, mwaka 1958 katika jiji la Kinshasa huko Congo na kupewa majina ya Mutomona Defao Lulendo. Alikuwa mwanamuziki mwenye kipaji cha kutunga na kuimba kwa sauti nyembamba na nyororo.

Defao alianza kujishughulisha na muziki mwaka 1976, akiwa katika bendi ya Orchestra Suka Movema kabla ya kuhamia Fogo Stars. Mwaka 1978 aliendа kupiga muziki katika bendi ya Korotoro huko Somo, Magharibi mwa Congo.

Alikuwa mmoja wa wanamuziki waliounda bendi mpya ya Grand Zaiko Wawa mwaka 1981, ikiongozwa na mpiga gita mashuhuri Pepe Felix Manuaku. Katika kile kilichoitwa mbinu za kujitafutia maisha, Defao aliungana na mwanamuziki Ben Nyamabo kuunda kikosi kipya cha Choc Stars.

Defao kwa kawaida alicheza sambamba na wanenguaji wake na alikuwa kivutio kikubwa cha wapenzi na mashabiki wake akicheza mitindo mbalimbali ukiwamo ule wa 'Ndombolo' pasipo kuchoka.

Ilipofika mwishoni mwa mwaka 1990, aliiacha bendi hiyo ya Choc Stars, akiwa na madhumuni ya kuunda bendi yake na akafanya hivyo kwa kuunda bendi yake iliyopewa jina la Big Stars. Katika bendi hiyo alipiga muziki kwa kushirikiana na mwimbaji mwingine Djo Poster, aliyetokea kwenye bendi ya Grand Zaiko.

Mifarakano katika sehemu za kazi huwa hazikosi na Big Stars iliyetetereka kwa kipindi kifupi baada ya kuondoka Djo Djo Bayenge na kumwacha Defao akiwa kiongozi wa bendi hiyo. Umaarufu wa General Defao ulizagaa maeneo mengi Afrika Mashariki na Kati kwenye miaka 1990. Wapenzi na mashabiki wake waliulinganisha umaarufu wake na ule wa wanamuziki kina Papa Wemba, Koffi Olomide, Bozi Boziana na Kester Emeneya.

Nyimbo kama Georgina, Fammilie Kikuta, Nadine, Bana Kongo, Oniva na Filie zilimpatia umaarufu mkubwa. Defao alilivunja kundi zima la Big Stars mwaka 2000 wakiwa katika Jiji la Kinshasa na yeye akaamua kwenda 'kutanua' katika Jiji la Paris, Ufaransa.

Katika hali isiyo ya kawaida, Defao baadaye akawa kimya katika anga za muziki. Hali hiyo yasemekana ilitokana na sintofahamu ya kisiasa nchini mwake iliyosababisha kufungiwa kupiga muziki huko kwao Congo. Defao alifika nchi za Afrika ya Mashariki ikiwamo Tanzania katika ziara yake ya hapa nchini iliyogubikwa na matatizo lukuki mwaka 2000.

Baada ya kumaliza kufanya maonyesho kadhaa, Defao alizidiwa akili na 'Mapromota' waliomleta, matokeo yake alifikia hadi kukosa fedha ya kujikimu pamoja na kulipia visa yake. Nguli huyo 'alifulia' hata nauli ya kumrejesha kwao Congo hakuwa nayo.

Bahati njema ilikuwa upande wake kwa kuwa alifanikiwa kurejea kwao baada ya kupewa 'lifti' katika ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATC), iliyokuwa ikizindua safari zake kati ya Dar es Salaam na Lubumbashi nchini DRC.

Kimya kingi kina mshindo mkuu. Usemi huu ulijionyesha wazi kwa gwiji huyo aliyesubiriwa na wapenzi kwa kipindi kirefu hadi mwaka 2006, ndipo alipotoka na albamu yake mpya yenye Lebo ya Nzombo le Soi. Baada ya miaka minne mingine alifyatua CD yake yenye Lebo ya Pur Encore mwaka 2010. Mwaka 2012 Defao kwa bahati nzuri alirudi ulingoni akiwa na album ya The Undertaker.

Hata mwaka jana na mwaka huu alitoa nyimbo ambazo zimetamba mno nchini Congo DR.

**Simu namba 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya siri-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WEWE unadhani ni kweli alimuua bosi wake?"

"Siamini." Lilikuwa ni jibu lililomshtua Eddy. Na moja kati ya jibu aliloliona la maana na alilolohitaji ni hilo.

"Kwa nini unadhani si kweli?"

"Sikiliza nikwambie." Alianza kuongea kwa sauti ndogo na kuonekana kuwa na wasiwasi, akiangalia huku na huko kama watu wapo karibu.

"Mimi nilimuona siku ile alipotoka duka la dawa. Si wanasema alimuua kwa dawa za dukani zilizochanganywa na kuwa sumu, siku ile nilimuona, alitoka kununua kwenye duka moja lipo mbele pale, alipofika hapo nje, akakutana na gari moja lilikuwa limesimama, nikaona kabisa anampa kile cheti na dawa, halafu yeye akarudi nyumbani, jamaa aliyekuwa kwenye gari akaondoka kuelekea sehemu nyingine."

Ilikuwa ni habari mpya kwa Eddy. Alianza kuona mwanga wa kile ambacho alikuwa anakihisi. Hata hivyo, bado kuna giza kubwa liliendelea kugubika, kwani hiyo yote haiondoi kuwa huenda Tina alishirikiana na huyo mtu. Lakini haiondoi wasiwasi wake kuwa kuna watu wapo nyuma ya mpango huu. Aliyoyasema mzee Mwayangu yalifanana na Nanje, ingawa kijana huyo alionekana kuwa na kitu kipya zaidi.

"Unamfahamu mtu huyo?"

"Hapana, ila mara moja moja huwa anapita na gari yake. Nina wasiwasi sana na mtu huyo."

"Ni gari ya aina gani?"

"Toyota Alphard ya rangi nyeupe."

Eddy alitoa noti tano za shilingi elfu kumi, na kumkabidhi kijana yule.

"Usimwambie mtu yeyote hii habari. Ila wewe si una simu ya tachi?"

"Ndiyo"


"Nakuomba ikipita ipige picha, ambayo namba zake zinaonekana wala usimpige dereva, halafu nitumie kwenye namba hii." Alimpa namba ya simu ambayo hutumia kwa masuala ya kijamii na si ya kikazi.

"Poa braza, nimekusikia, nitaifanya kazi hii, yaani umenipiga tafu sana na hii pesa."

************************************

"Hujambo bibi?" Alisalimia Eddy baada ya kupigiwa simu.

"Sijambo, nashukuru sana kwa hela uliyonitumia jana, kiukweli sikutegemea."




**Ilikuwa ni habari mpya kwa Eddy. Alianza kuona mwanga wa kile ambacho alikuwa anakihisi. Hata hivyo, bado kuna giza kubwa liliendelea kugubika, kwani hiyo yote haiondoi kuwa huenda Tina alishirikiana na huyo mtu.**

Eddy aliangua kicheko kifupi, halafu akasema.

"Yaani mimi nikudanganye?"

"We huwajui baadhi ya wanaume wewe, yaani anaweza kukuahidi vizuri, halafu kama utamuona."

"Kati ya hao mimi simo." Alijibu Eddy na kusababisha aliyekuwa anaongea naye aangue kicheko.

"Ni kweli nimeamini humo."

Ilikuwa ni sauti ya Mwahija. Usiku wa saa sita usiku, Eddy alimtumia kiasi cha 50,000, ikiwa ni ahadi ya pesa ya kusuka, baada ya kukutana kwa mara ya kwanza na kumuahidi kwa utani kuwa atampa pesa ya kusukia, baada ya kumsifia kuwa amependeza.

"Kakusuka nani hizi nywele?"

"Mhh, nimesuka kwenye saluni ya hapo nyuma tu."

"Najua siku mbili tatu utafumua. Sasa nataka ukifumua uende kwenye saluni hii hii na msusi huyu huyu, akusuke hivi hivi, halafu mimi ndiyo nitalipa, unasikia?"

"Mhhh, yaani utakuja tena huku?"

"Kwanini nisije? Ukiniambia tu tayari nimeshasuka, basi mimi nakuja huku huku kulipa." "Haya bwana, nitakwambia."

Yalikuwa ni maneno ambayo Eddy anayakumbuka aliyatumia kumsifia Mwahija kwa ajili ya kumtuliza, kutokana na jinsi alivyopokelewa siku ile pale kwenye duka la madawa.

Ni maneno yaliyotengeneza ukaribu ambao haukuwapo mwanzo. Pia ulimfanya Mwahija kujibu kila alichokuwa anahitaji Eddy kujibiwa.

"Umesuka vile vile ulivyosuka siku ile, au umebadilisha mtindo?" Aliuliza tena.

"Si ulinimbia vile vile, halafu utakuja kuniona, nimesuka vile vile."

"Ila samahani, maana pesa nimetuma usiku sana, pamoja na meseji kuwa usinipigie simu hadi ukimaliza kusuka. Sasa nilikuwa na wasiwasi inaweza kuonwa na mtu mwingine."

Mwahija aliangua kicheko. "Mwingine nani? Mi naishi kwa mama yangu mdogo."

"Mwahija wee, urembo wote huo huna mtu kweli?. Hunifungi kamba kweli?"

"Wanaoninyatia huwa hawakosekani, wengi tu, lakini mimi kama mwanamke lazima niwe na msimamo, nitafute mtu wa kweli, mpenzi wa kweli, mwenye msimamo, siyo ambaye anataka tu kukuchezea, halafu akutupe, aende kwa wengine, huku ni kuumizana na kupotezeana muda." Alijibu Mwahija na hisia.

"Ahaa, ndiyo maana siku ile nilipokuja pale ofisini kwenu na kusema namtaka Mwahija ukawa mkali, na kunitazama kama mama anayemwangalia mtoto wake aliyepoteza pesa aliyopewa akanunue unga dukani." Ni jibu lililomfanya Mwahija kukauka kwa kucheka.

"Na wewe nawe husahau tu, nimekwambia samahani."

"Basi tuachane na hayo." Eddy alibadilisha mada. "Si umeshasuka? Kesho utakuwa na nafasi nataka tule chakula cha jioni mimi na wewe."

"Okay, wapi?"

"Kwani wewe unaishi wapi?"

"Mimi naishi huku huku Tegeta."

"Basi nisikupeleka mbali sana, tukutane Kunduchi saa moja usiku. Kuna pub mpya pale inaitwa Fabrice, maarufu sana."

"Ahsante sana, nitakuja."

************************************

Alikuwa ndani ya pub hiyo dakika 20 kabla ya saa 1:00 usiku. Ni kawaida kwa mtu kama yeye. Nia ni kuangalia usalama.

Kama kawaida alitafuta eneo la nyuma linaloangalia mlango mkuu. Alinyanyuka kuelekea msalani. Kabla ya kufika huko alishtuka. Kuna kitu kilimshtua ambacho hata mwenyewe hakuelewa mara moja ni kitu gani.

Njia ya kwenda msalani pembeni yake kulikuwa na sehemu ya kuegeshea magari.

Gari lenye rangi nyeupe aina ya Toyota Alphard ilionekana kupaki maeneo hayo. Sasa akakumbuka kuwa kilichomsimamisha ni kuifananisha gari hiyo.

Alisubiri hadi dereva wa gari hilo ameteremka. Alikuwa ni kijana ambaye anaonekana huenda ana umri kati ya miaka 26 mpaka 30 hivi. Alivaa suruali aina ya jeans na fulana ya rangi ya bluu.

Alishuka ndani ya gari hiyo peke yake. Bila hili wala lile aliingia kwenye pub hiyo.

Eddy alitoka nje na kujifanya kama vile anaondoka. Alijifanya kama analifuata gari lake. Haikuwa hivyo. Alikuwa akiliangalia kwa makini gari lile. Hakumuhitaji dereva. Alilitaka gari lake.

Akaziangalia na kuzisoma namba za gari lile kwa kichwa. Akaingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi. Akatafuta picha moja akaiangalia. Ilikuwa ni picha ya gari lile. Na namba zilikuwa ni zile zile. Aliisaka picha nyingine aliyokuwa na wasiwasi nayo. Nayo ilikuwa picha ya gari lile lile. Ni kwa sababu namba zilikuwa ni zile zile. Akatabasamu. Akafungua mlango wa gari yake na kujifanya kama anatafuta kitu ili kusiwe na mtu ambaye atamshuku. Akaufunga na kurejea tena kwenye pub. Akalipita tena gari lile. Akazisoma tena namba, huku kwa uangalifu wa hali ya juu akalipiga picha kwa simu yake ya mkononi.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# HUYU NDIYE MTAALAMU YOGO MWENYE MIKONO YA DHAHABU

WENGI hawamfahamu kwa undani, lakini ndiye mpishi wa nyimbo zote za Mfalme wa Bongo Fleva nchini, Ali Kiba ambazo zinafanya vizuri barani Afrika.

Yogo ni prodyuza wa muziki anayefanya kazi zake kwa umakini kiasi cha Ali Kiba, kushindwa kuvumilia na kumtaja kwamba ni namba moja kwa kutengeneza ngoma kali kwa mwaka 2021.

Ikumbukwe kuwa Yogo amehusika kuitengeneza album ya Alikiba ya 'Only one King' ambayo ina ngoma 16, pia ametengeneza nyimbo za wasanii wengi wa lebo ya Kings Music.

## Jitu Baya atoa zawadi Mwaka Mpya

RAPA mkali Jitu Baya, amewapa mashabiki wake zawadi ya Krismasi na Mwaka Mpya ya nyimbo inayoitwa 'Chapa' ambayo ameiachilia hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe, Jitu Baya , amesema wimbo huo ambao ameutambulisha kwa mashabiki zake siku ya 'Boxing day'utakuwa asante yake kwa wale wanaomuunga mkono katika kazi yake ya muziki.

"Mashabiki zangu nawaheshimu sana na nimewapa zawadi hii ya wimbo 'Chapa', nawashukuru kwa kuniunga mkono kwa mwaka mzima na tuendelee kuwa pamoja kwa miaka mingi ijayo," amesema.





## Omashola amchumbia mpenzi wake chini ya maji

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), Omashola, amefanya tukio la kipekee baada ya kumvisha pete ya uchumba mpenzi wake wakiwa ndani ya maji.

Nyota huyo wa runinga, amefanya tukio hilo usiku wa kuamkia mwaka mpya na video yake akaiweka katika akaunti yake ya Instagram.

"2021 ulikuwa na siri nyingi, lakini kubwa zaidi ni pale aliponitamkia ndiyo na kufunga historia. Tafadhali usiniulize nini kinaendelea nawatakia heri ya mwaka mpya," ameandika Omashola.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### SPURS YAMTAKA COUTINHO

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mchezaji nyota wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho, 29, kwa uhamisho huru. ***(El Nacional)***

#### ALVAREZ ANUKIA UNITED

MANCHESTER United iko tayari kulipa pauni milioni 16.8 zinazohitajika kwa ajili ya kipengele cha mkataba kitakachowawezesha kumsajili mshambuliaji wa River Plate, Julian Alvarez, 21, katika dirisha hili la Januari. ***(Sport)***

#### NEWCASTLE YAZIDI KUKOMAA

NEWCASTLE inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mlinzi wa kulia wa Atletico Madrid, Kieran Trippier, 31. ***(Athletic)***

#### RUDIGER KUIKAMUA CHELSEA

CHELSEA watalazimika kutoa ofa ya mshahara mkubwa kwa mlinzi wa kati wa Ujerumani, Antonio Rudiger, (28), ambaye atakuwa akilipwa mshahara mkubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote wa Blues ili kumshawishi aongeze mkataba mpya. ***(Football Insider)***

#### TRAORE ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur bado inaendelea kumsaka mshambuliaji wa Wolves na Hispania, Adama Traore, 25. ***(Fabrizio Romano via This is Futbol)***

#### SIONI KUTUA NORWICH

NORWICH wanaangalia uwezekano wa kuwasajili mlinzi wa kulia, Sion na beki, 26, Guadeloupe Dimitri Cavare, ili kuziba pengo la Max Aarons, ambaye anaendelea kuhusishwa na taarifa za kujiunga na Carrow Road. ***(Jeunes Footeux via Norfolk Live)***

#### BRAAF NJIA MOJA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kumruhusu winga anayetazamiwa kufanya vyema siku zijazo, Jayden Braaf, 19, kuondoka kwenye klabu hiyo hii Januari. ***(Manchester Evening News)***

#### ROBERTS KWENDA SUNDERLAND

SUNDERLAND inakaribia kukamilisha mkataba na winga wa Manchester City mwenye umri wa miaka, 24 Patrick Roberts. Raia huyo wa England kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Troyes iliyoko Ufaransa. ***(Football Insider)***

#### ISAK KUTUA ARSENAL

ARSENAL imewatambua nyota wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, na nyota wa Lille na Canada, Jonathan David (21), kama chaguo linalowezekana ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(The Athletic)***

#### TCHOUAMENI KUTUA EPL

CHELSEA inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Monaco, Mfaransa Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaweza kuwa chaguo nafuu kuliko nyota wa West Ham na England, Declan Rice (22). ***(Daily Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU HAFURAHII MAISHA YA CHELSEA

### Ni kutokana na mfumo wa Tuchel, lakini aweka wazi anatamani kurejea Inter huku...

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Romelu Lukaku, ameamua kuweka wazi hafurahishwi na mfumo unaotumiwa na kocha wake, Thomas Tuchel ndani ya klabu hiyo.

Lukaku ameenda mbali zaidi na kusema hana furaha ndani ya klabu hiyo na ipo siku atarejea katika timu yake ya Inter Milan huku akijutia haelewi ni uamuzi gani wa kuondoka alioufanya.

**"Utimamu wa kimwili nipo sawa . Lakini sina furaha na hali ilivyo ndani ya Chelsea. Tuchel ameamua kucheza na mfumo mwingine, sitokata tamaa, sina furaha na hali ilivyo lakini nitabaki kutimiza majukumu yangu," amesema Lukaku.**

"Ni matumaini yangu kutoka moyoni kabisa nitarejea Inter Milan sio wakati nikiwa mwisho wa maisha yangu ya soka bali bado nikiwa katika ubora wangu.

"Nataka kuomba msamaha kwa mashabiki wa Inter, muda ambao nilizungumza maneno yangu haukuwa sahihi, mlichonifanyia kitabaki milele kwenye moyo wangu.

"Huu ni muda sahihi wa kuwaambia hisia zangu, mara zote huwa nasema Inter ipo moyoni mwangu, najua nitarejea, naipenda Italia, huu ni muda sahihi wa kuongea na kuwafahamisha watu nini kilitokea."

MECHI KALI
HOME
AWAY
CHELSEA
2.71 | 3.41 | 2.51
LIVERPOOL

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 804

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WATATU WATAJWA KUMRITHI AZPILICUETA



**LONDON,** England

CHELSEA imeripotiwa kuandaa orodha ya wachezaji watatu wenye uwezo wa kuchukua nafasi ya beki wake wa pembeni, Cesar Azpilicueta wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Azpilicueta anaonekana kujiandaa kujiunga na 'wababe' wa Katalunya mwishoni mwa msimu huu mkataba wake utakapomalizika pale Stamford Bridge.

Inaaminika Barcelona tayari ina makubaliano na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alifika Chelsea mwaka 2012 na ametoa asisti 56 katika michezo 450 aliyocheza.

Hii ina maana ataacha pengo kubwa kwenye kikosi cha kocha, Thomas Tuchel akiondoka.

Kwa mujibu wa Express, mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya watawalenga, Jules Kounde wa Sevilla, Attila Szalai wa Fenerbahce na Maxence Lacroix wa Wolfsburg kama mbadala wa Azpilicueta.

Real Madrid na Manchester United pia wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumnunua Kounde, lakini iliripotiwa wiki iliyopita kuwa Blues hao tayari wana makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.



# Barcelona watia nia kwa De Ligt

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi kwa kumsajili, Matthijs de Ligt kutoka Juventus, kwa mujibu wa ripoti ya Diario Sport.

Kipaumbele cha Blaugrana hao kwa soko lililobaki la usajili la Januari ni kusonga mbele na kupunguza bajeti yao ya mishahara, lakini tayari wanatazamia ununuzi wa msimu wa joto.

Inasemekana kocha Xavi anavutiwa na De Ligt, ambaye alijiunga na Juventus kutoka Ajax msimu ambao Barcelona ilimsajili swahiba wake, Frenkie de Jong.

Kifungu cha kuachiwa kwa [De] Ligt kule Turin ni euro milioni [...] na inaeleweka kuwa Juventus [wa]nataka kurudisha euro milion[i ...] walizoilipa Ajax.

Kuna imani pia wakala wa de [Ligt,] Mino Raiola ameiambia Barce[lona] kwamba ana kifungu cha kuond[oka] kilichojadiliwa na Juventus ha[...] kwa ajili yao ambacho ni chin[i ya] euro milioni 125.

De Ligt mwenye miaka 22, am[e...] mia maisha yake yote akiwa na [...] kabla ya kwenda Serie A na a[me]chezea Timu ya Taifa ya Uhol[anzi] michezo 33.

4,667,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/01/22 | 17:00 | Brentford vs Aston Villa | 2.96 | 3.26 | 2.41 |
| 02. 02/01/22 | 17:00 | Everton vs Brighton | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 02/01/22 | 17:00 | Birmingham vs QPR | 2.57 | 3.11 | 2.71 |
| 04. 02/01/22 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.47 | 3.25 | 2.76 |
| 05. 02/01/22 | 18:00 | Queen of South vs Hamilton | 2.49 | 3.28 | 2.64 |
| 06. 02/01/22 | 18:00 | Arbroath vs Inverness | 2.44 | 3.09 | 2.84 |
| 07. 02/01/22 | 18:00 | Alloa Athletic vs Falkirk FC | 2.74 | 3.22 | 2.44 |
| 08. 02/01/22 | 18:00 | Stenhousemuir vs Stirling | 2.34 | 3.38 | 2.66 |
| 09. 02/01/22 | 18:15 | Elche vs Granada | 2.47 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 02/01/22 | 19:30 | Chelsea vs Liverpool | 2.95 | 3.45 | 2.32 |
| 11. 02/01/22 | 20:30 | Alaves vs Real Sociedad | 3.36 | 3.11 | 2.27 |
| 12. 02/01/22 | 23:00 | Mallorca vs Barcelona | 3.30 | 3.21 | 2.24 |
| 13. 02/01/22 | 23:00 | Fuenlabrada vs UD Ibiza Eivissa | 2.27 | 2.95 | 3.34 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 02 - JANUARI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:45 | 4877 | Cannes vs Toulouse | 6.33 | 4.75 | 1.42 |
| 15:45 | 5986 | Nantes vs AS Vitre | 1.16 | 7.13 | 13.87 |
| 16:00 | 4660 | Almeria vs FC Cartagena | 1.61 | 3.79 | 5.11 |
| 16:00 | 5100 | RC Arbaa vs CS Constantine | 2.80 | 2.85 | 2.56 |
| 16:00 | 5364 | Getafe vs Real Madrid | 5.14 | 3.66 | 1.69 |
| 16:00 | 5516 | Valladolid vs Leganes | 1.99 | 3.24 | 3.73 |
| 16:00 | 5529 | Bristol City vs Millwall | 2.93 | 3.13 | 2.39 |
| 17:00 | 1831 | Everton vs Brighton | 2.80 | 3.15 | 2.60 |
| 17:00 | 2175 | Brentford vs Aston Villa | 3.06 | 3.26 | 2.35 |
| 17:00 | 2259 | Birmingham vs QPR | 2.49 | 3.13 | 2.79 |
| 17:00 | 2486 | Leeds vs Burnley | 2.00 | 3.60 | 3.55 |
| 17:00 | 2568 | West Bromwich vs Cardiff | 1.45 | 4.13 | 6.68 |
| 17:00 | 4446 | Blackburn vs Huddersfield | 1.78 | 3.54 | 4.23 |
| 18:00 | 1102 | Morecambe vs Doncaster | 2.04 | 3.34 | 3.44 |
| 18:00 | 1153 | Sporting Gijon vs Lugo | 1.92 | 3.23 | 4.01 |
| 18:00 | 1180 | Nancy vs Rennes | 6.12 | 4.24 | 1.48 |
| 18:00 | 1452 | Woking vs Aldershot | 2.32 | 3.32 | 2.83 |
| 18:00 | 1914 | Notts County vs Wrexham | 2.60 | 3.24 | 2.55 |
| 18:00 | 1948 | Bastia vs Clermont Foot | 3.35 | 3.30 | 2.12 |
| 18:00 | 2279 | Raith Rovers vs Dunfermline | 1.91 | 3.51 | 3.61 |
| 18:00 | 2399 | Montpellier vs Strasbourg | 2.45 | 3.21 | 2.82 |
| 18:00 | 2432 | Maidenhead U vs Wealdstone | 2.17 | 3.33 | 3.08 |
| 18:00 | 2490 | Boreham Wood vs Barnet | 1.70 | 3.71 | 4.40 |
| 18:00 | 2628 | Eastleigh vs Weymouth | 1.60 | 3.80 | 5.07 |
| 18:00 | 4194 | Dagenham and Redbridge vs Dover | 1.21 | 5.84 | 11.68 |
| 18:00 | 4336 | Arbroath vs Inverness | 2.45 | 3.08 | 2.84 |
| 18:00 | 4588 | Shrewsbury vs Sheffield Wed | 3.13 | 3.23 | 2.21 |
| 18:00 | 4833 | Partick Thisle vs Morton | 1.61 | 3.83 | 4.91 |
| 18:00 | 5067 | Yeovil vs Torquay | 2.32 | 3.21 | 2.92 |
| 18:00 | 5523 | Queen of South vs Hamilton | 2.49 | 3.28 | 2.64 |
| 18:15 | 3440 | Atletico Madrid vs Rayo Vallecano | 1.33 | 4.90 | 9.60 |
| 18:15 | 4995 | Elche vs Granada | 2.48 | 3.10 | 3.00 |
| 19:00 | 5679 | JS Saoura vs MC Alger | 1.90 | 3.04 | 4.06 |
| 19:30 | 5770 | Chelsea vs Liverpool | 2.71 | 3.41 | 2.51 |
| 20:00 | 3664 | ES Setif vs Ol. Medea | 1.54 | 3.33 | 6.56 |
| 20:15 | 1008 | Huesca vs Girona | 2.56 | 3.00 | 2.81 |
| 20:15 | 3365 | Mirandes vs Zaragoza | 3.39 | 3.10 | 2.16 |
| 20:30 | 1511 | US Quevilly Rouen vs Monaco | 7.10 | 4.54 | 1.40 |
| 20:30 | 1718 | Alaves vs Real Sociedad | 3.40 | 3.10 | 2.25 |
| 20:30 | 3232 | Linas Monthlery Esa vs Amiens | 4.66 | 3.96 | 1.64 |
| 20:30 | 3311 | Betis vs Celta Vigo | 1.76 | 3.79 | 4.39 |
| 20:30 | 3691 | ES Thaon vs Reims | 10.90 | 6.14 | 1.22 |
| 20:30 | 5036 | Jura Sud-Lavans vs St Etienne | 7.07 | 5.11 | 1.36 |
| 21:15 | 5047 | Hapoel Beer Sheva vs Bnei Sakhnin | 1.50 | 3.86 | 5.79 |
| 21:30 | 2652 | FC Vizela vs Belenenses | 1.95 | 3.35 | 3.79 |
| 22:30 | 3964 | FAR Rabat vs Raja Casablanca | 2.59 | 2.98 | 2.64 |
| 23:00 | 1203 | Mallorca vs Barcelona | 3.30 | 3.20 | 2.25 |
| 23:00 | 3771 | US Chauvigny vs Marseille | 20.66 | 7.87 | 1.11 |
| 23:00 | 5370 | Fuenlabrada vs UD Ibiza Eivissa | 2.27 | 2.95 | 3.34 |
| 23:30 | 3740 | Tenerife vs Las Palmas UD | 2.14 | 3.10 | 3.45 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KOCHA BIASHARA UNITED AKARIBIA KUTUA GEITA FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo amesema yuko katika mazungumzo na mabosi wa Geita Gold FC inayoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ili kurithi nafasi iliyoachwa na Mrundi Etienne Ndayiragije.

**Odhiambo amevunja mkataba wake na Biashara United baada ya kuona mambo hayaendi sawa sawa kwenye timu hiyo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema yuko katika hatua za mwisho za mazungumzo hayo na mambo yakienda sawa atarejea Tanzania hivi karibuni ili kujiunga na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu.

"Ni kweli ninazungumza na Geita Gold FC ila kwa sasa sitaweza kusema lolote kuhusu mazungumzo hayo, mambo yakienda sawa sawa ninatarajia kurejea Tanzania wiki ijayo," alisema Odhiambo ambaye yuko kwao Kenya kwa mapumziko mafupi.

Naye Katibu Mkuu wa Geita Gold FC, Shija Simon, alisema hizo ni tetesi na kwa sasa hawana mpango huo kwa sababu wanaimani na Kaimu Kocha Mkuu, Fred Minziro, ambaye anaisimamia timu yao.

Shija alisema kwa sasa timu yao inafanya vizuri baada ya kubakia Minziro na matokeo hayo mazuri yamefanya wasiwaze kutafuta kocha mpya.

"Kuhusu Odhiambo hizo ni tetesi tu hakuna ukweli wowote, kwa mwenendo wa timu yetu chini ya Minziro ni mzuri kwa sasa kwa hali hiyo hatujafikia kutafuta kocha mkuu," alisema Shija.

Geita iliamua kuachana na Ndayiragije baada ya timu hiyo kutopata matokeo mazuri katika baadhi ya michezo ya mwanzoni mwa msimu huu.





Waimbaji wa Kwaya ya Dar es Salaam Unity Praise Worship Team wakiimba wakati wa mkesha wa Tamasha la kuukaribisha mwaka mpya wa 2022 lililofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Namungo, Meli 4 kibaruani Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Meli 4 City inatarajia kuikaribisha Namungo FC katika mechi ya Kundi A ya ufunguzi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi, Aiman Duwe, aliliambia gazeti hili jana maandalizi yote kuelekea michuano hiyo inayofanyika kila mwaka yamekamilika.

Aiman alisema timu zinazoshiriki michuano hiyo kutoka Tanzania Bara zitaanza kuwasili Zanzibar kuanzia kesho huku wawakilishi kutoka Pemba tayari wameshafika kituoni.

"Tunatarajia kuwa na mashindano yenye ubora, timu zote 10 zitakazoshiriki michuano hii kutoka Tanzania Bara na Visiwani zina vikosi imara na zimejipanga kuonyesha ushindani," alisema Aiman.

Mashindano hayo yataendelea tena kesho kwa Selem View kuwakaribisha Mlandege wakati Taifa Jang'ombe itacheza dhidi ya KMKM.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi watashuka dimbani Januari 5, mwaka huu kuwakabili Taifa Jang'ombe wakati Selem View itacheza dhidi ya Simba.

# Michezo

Jumapili Januari 2, 2022

Nipashe



Lukaku hafurahii maisha ya Chelsea UKURASA 21

MAUAJI...



Kiungo wa Yanga, Saido Ntibazonkiza (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 4-0.
**PICHA : JUMANNE JUMA**

## Simba yafunguka majembe mapya

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kiungo Mzambia, Clatous Chama anatarajiwa kutua nchini muda wowote kurejea katika timu yake ya zamani ya Simba, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco amesema anahitaji wachezaji wapya watakaosajiliwa wawe na uwezo wa ziada ili kuwasaidia mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kufikia malengo.

Pablo alisema anataka wachezaji wapya wawe na uwezo wa kuingia kwenye kikosi cha kwanza moja kwa moja ili kuipa timu matokeo chanya inayohitaji.

Mhispania alisema haoni sababu ya timu kuwa na kundi kubwa la wachezaji, wengine wakiwa hawatumiki ipasavyo, hivyo anahitaji kikosi cha wachezaji wachache watakaotumika pale wanapohitajika kufanya hivyo.

"Nimeona na kusoma kwenye mitandao ya kijamii zaidi ya wachezaji 26 wanatajwa wanakuja Simba kutoka nchi mbalimbali (Cameroon, Zambia), lakini hiyo ni mitandao ya kijamii na uvumi, kwangu nimehitaji wachezaji angalau wanne tu wenye uwezo mkubwa zaidi ya kuibadilisha timu kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo," alisema Pablo.

Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, alisema mpaka jana hawajawa tayari kutoa taarifa kamili ya wachezaji wapya waliosajiliwa lakini mchakato huo unaelekea ukingoni.

Mangungu alisema Simba inaendelea kufanya usajili wake kwa umakini kwa sababu inahitaji kutimiza malengo ya kusonga mbele kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA.

Chama ambaye aliuzwa katika timu ya RS Berkane ya Morocco anatajwa kurejea nchini wakati wowote baada ya Simba na Waarabu hao kumalizana.

# *Nabi atarajia makubwa Yanga*

### ●●● Kocha huyo asema kiwango cha sasa kinachoonyeshwa ni asilimia...

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 4-0, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema idadi kubwa ya mabao ambayo kikosi chake kimepata dhidi ya Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi haimaanishi wachezaji wake wamefikia ubora anaouhitaji.

**Ushindi huo umeifanya Yanga kufikisha pointi 29 na kujiimarisha kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ambayo watani zao, Simba ndio mabingwa watetezi.**

Nabi alisema bado wachezaji wake hawajafikia kiwango cha asilimia 100 ambacho anakihitaji kukiona kwenye mechi za ligi na mashindano mengine ya hapa nchini wanayoshiriki.

Kocha huyo alisema kupata idadi kubwa ya mabao haitoshi kumridhisha kwamba timu yake imekuwa bora kwa sababu dakika za mwanzo wa mchezo walionekana kuzidiwa na wapinzani ambao walionyesha kandanda safi.

"Hatujafikia ubora ambao ninauhitaji ndani ya kikosi chetu, ingawa tunashinda na tumeanza kupata mabao mengi, lakini angalia dakika za mwanzo hatukuwa vizuri, wapinzani wetu walicheza mpira mzuri na walimudu kutuzuia," alisema Nabi.

Alisema kutokana na aina ya mpira waliocheza Dodoma jiji FC, alilazimika kuwaambia wachezaji wake wabadili mfumo kwa kucheza mpira wa kukimbiza ambao ulilenga kuwachosha na hatimaye Yanga ilitumia mapungufu hayo.

"Hadi sasa tuko asilimia 60 ingawa tumepata ushindi wa mabao haya 4-0, hii ilitokana na mafanikio ya mbinu zetu, wao walizuia sana na sisi tukawachosha kwa mbio na kufanikiwa kupata bao la kwanza, na wao walikaribia kusawazisha.

"Wapinzani hawakuwa dhaifu, wao walitaka kusawazisha na kufunga, lakini walijisahau na kuacha nafasi ambazo tulizitumia kutafuta mabao na kufanikiwa kwa mbinu zetu tulizokuwa nazo," alisema Nabi.

Aliongeza aliamua kumpa nafasi ya kucheza kiungo wake mpya, Salum Abubakar 'Sure Boy' kwa lengo la kumtambulisha kwa mashabiki na kumkaribisha ndani ya kikosi hicho chenye kiu ya kutwaa taji la ligi hiyo.

"Sure Boy ni mchezaji mzuri na ana ubora kama ilivyo kwa Khalid Aucho katika utekelezaji wa majukumu kwenye eneo la kiungo, nimefurahia usajili huu, kikosi kimekamilika sehemu ya kiungo, Sure Boy alionyesha ni mtu sahihi wa kuziba nafasi ya Aucho atakapokosekana," alisema Nabi.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Makata, alisema wachezaji wake hawakuwa bora katika mechi hiyo baada ya kufanya makosa mengi hasa kwenye nafasi ya ulinzi.

"Hatukuwa vizuri, tulicheza chini ya kiwango chetu kilichozoeleka, hasa nafasi ya kiungo mkabaji, mabeki hawakutekeleza majukumu yao na waliwapa nafasi Yanga ya kutuadhibu," alisema Makata.

Alikiri wachezaji wake walifanya makosa ya kujirudia na Yanga walitumia vyema nafasi hiyo kuwashambulia mara kwa mara langoni mwao.

"Baada ya kucheza vizuri dakika 35 za kipindi cha kwanza, mabeki na viungo wangu walifanya makosa na Yanga walitumia nafasi hiyo kutuadhibu, Yanga walikuwa bora zaidi yetu na walistahili kuibuka na ushindi huo wa idadi kubwa ya mabao ambayo kwetu ndio mara ya kwanza kufungwa idadi hiyo," Makata alisema.

Alimalizia kwa kusema matokeo hayo yanawarudisha darasani kujiimarisha ili ligi itakaporejea kuanzia Januari 14, mwaka huu wawe imara kwa mapambano.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 3 9